


**Avamiwa** na kujeruhiwa na fisi, ang'olewa sehemu nyeti

UKURASA 3




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Mei 22, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581318

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


## RIPOTI MAALUM:

# Urafiki kutoka kiwanda hadi godauni, maegesho

• **Nyumba** za wafanyakazi zageuzwa ofisi, ukumbi kanisa...

*Endelea ukurasa 4*



Mwonekano wa eneo lililokuwa na mitambo katika Kiwanda cha Nguo cha Urafiki ambalo limegeuzwa kuwa ghala la kuhifadhia bidhaa, matrekta, vioo na vitu vingine vya wafanyabiashara na wachuuzi kutoka nje ya nchi.

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### TANZANIA YATEULIWA KUINGIA KAMISHENI YA TAKWIMU UN

TANZANIA imeteuliwa kuingia kwenye Kamisheni ya Takwimu ya Umoja wa...

UKURASA WA 3

### MAZUNGUMZO SERIKALI, SHELL GESI YAKAMILIKA

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema mazungumzo na kampuni...

UKURASA WA 5

### UFARANSA YAFUNGUA MILANGO UTALII TANZANIA

BODI ya Utalii Tanzania (TTB), imesema hali ya utalii nchini inaendelea...

## Wauguzi wamvaa mkurugenzi fedha za sare kazini

UKURASA 2



Gari la kubeba bidhaa baada ya kushusha mizigo na kushoto ni gari lililoshusha vioo. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

## Wamiliki wa shule walia na utitiri wa kodi, tozo

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA NI MAYELE, MAYELE NI YANGA UK.24 **KATUNI** UK.6

## Tanzania yateuliwa kuingia Kamisheni ya Takwimu UN

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TANZANIA imeteuliwa kuingia kwenye Kamisheni ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwakani hadi 2027.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), kufanya vizuri kwenye Kamisheni ya Takwimu Afrika kama Mwenyekiti kwa vipindi viwili mfululizo hadi mwaka 2021.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema hayo wakati akitoa taarifa kwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, kwenye ufunguzi wa kikao cha tatu cha Baraza la Sita la Wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu kinachofanyika mjini Morogoro.

Dk. Chuwa alisema Kamisheni ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa inaundwa na nchi 23 na kwamba kuongezeka kwa Tanzania kutafanya jumla kuwa 24.

Kwa mujibu wa Dk. Chuwa, mafanikio hayo yanatokana na utashi wa kisiasa wa Rais Samia Suluhu Hassan katika masuala ya kitakwimu pamoja na kufanya vizuri kwa matokeo ya mwanzo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

Alisema kutokana na heshima hiyo, ahadi ya NBS kwa serikali ni kuhakikisha inaendelea kufanya kazi vizuri, kwa bidii na weledi, ili kuimarisha ushirikiano na wadau wake kwa kuzalisha takwimu bora na kwa wakati, katika kukidhi mahitaji ya takwimu.

NBS, ilisema imeanza kuweka mazingira mapya ya shughuli za kitakwimu kwa kuongeza matumizi ya teknolojia katika ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu pamoja na maeneo mapya ya tasnia ya takwimu kama takwimu za sayansi ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya takwimu.

Akifungua baraza hilo, Naibu Waziri Chande alisema serikali inajivunia NBS kutokana na utendaji wake mzuri wa kazi ndani na nje ya nchi na kuiletea sifa nchi na kwamba wengine wanakwenda kujifunza.

Alisema pamoja na NBS kufanya vizuri imekuwa ikitekeleza kwa vitendo agizo la Rais Namba Moja la mwaka 1970, Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 kuhusu umuhimu wa kuimarisha uhusiano mahali pa kazi kupitia vikao vya baraza la wafanyakazi.

Aidha, aliipongeza NBS kwa uteuzi huo ambao umetokana na kazi nzuri, na kwamba wamezidi kuipaisha Tanzania kimataifa.



Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan akiongoza kikao cha Kamati Kuu ya chama hicho, Ikulu Chamwino jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Wamiliki shule walia utitiri wa kodi

**Na Joseph Mwendapole**

MBUNGE wa Bukoba Vijijini (CCM), Dk. Jasson Rweikiza, amesema wamiliki wa shule wametwishwa mzigo mkubwa wa kodi kutokana na kulipa aina 18 za tozo.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Rweikiza ambaye ni mmoja wa wamiliki wa shule binafsi, ameiomba serikali kuwapunguzia kodi kwa kuwa zimekuwa zikisababisha mzigo kwa wazazi na walezi.

Alitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki Dar es Salaam wakati wa mahafali ya 15 ya kidato cha sita katika Shule ya St, Marie Academy yaliyofanyika shuleni hapo, Mbezi kwa Msuguri.

Dk. Rweikiza ambaye ni Mkurugenzi wa Shule hiyo, alisema wamiliki wa shule wanalipa kodi 18 hali inayofanya kiwango cha ada kuwa juu, hivyo kuwabebesha mzigo wazazi.

Alisema iwapo kodi hiyo itapungua, ada nayo inaweza kushuka, hivyo kuwapunguzia mzigo wazazi na kwamba kupungua kwa ada kutasababisha wanafunzi wengi kupata fursa ya elimu bora.

"Serikali inatoa elimu bure lakini sisi wa shule binafsi tunatozwa kodi nyingi sana, michango ya manispaa, kata, kodi za moto na leseni mbalimbali za halmashauri ni baadhi ya tozo tunazolipa. Tunaomba zipunguzwe kwa maana ya kuwapunguzia mzigo wazazi," alisema Dk. Rweikiza.

Wakati huo huo, Dk. Rweikiza aliahidi kutoa simu ya iphone macho matatu kwa wanafunzi wa kidato cha sita watakaopata daraja la kwanza kwenye mitihani ya kidato cha sita.

Dk. Rweikiza alisema kwa namna wanafunzi hao walivyoandaliwa na kupata matokeo mazuri kwenye mitihani ya majaribio ana matumaini kwamba asilimia kubwa watapata daraja la kwanza.

"Nimeahidi iphone macho matatu lakini kutokana na namna mlivyoandaliwa nimeanza kuwa na wasiwasi kwamba iwapo wote mtapata Division One nitapata wapi fedha za kuwanunulia iphone nyinyi wote ila kwa kuwa ni ahadi nitajitahidi kuitekeleza," alisema.

Alisema matokeo mazuri ya shule hiyo yanatokana na mazingira mazuri ya kusomea ikiwamo chakula kizuri, maji ya uhakika na umeme na maktaba za kisasa na walimu mahiri.

Pia alisema shule imeendelea kuhakikisha inakuwa na madarasa bora na ya kutosha ili darasa likae na wanafunzi wachache kumwezesha mwalimu kumiliki darasa vizuri ili wanafunzi wamwelewe.

Alisema shule hiyo ina maktaba nzuri iliyosheheni vitabu vingi vya kiada na ziada na mazingira safi ya kusomea kama viyoyozi na huduma ya afya ya uhakika kwa wanafunzi.

Dk. Rweikiza alisema shule imeendelea kujiimarisha zaidi na imeweka uzio eneo lote la shule na ina askari wa kutosha wenye mafunzo na uwezo wa kutumia silaha za moto pamoja na mbwa wakali kwa ajili ya ulinzi wa shule.

Alisema kutokana na sababu za kuwapo kwa majanga ya moto kwenye maeneo mbalimbali shule imechukua tahadhari ya kujikinga na ajali zitokanazo na moto kwa kuweka vifaa vya kuzimia moto.

Dk. Rweikiza alirudia ahadi yake kwamba hakuna mwanafunzi wa shule zake ambaye atafukuzwa shule iwapo atafiwa na wazazi akiwa anasoma kwenye shule hizo.

"Hii ni ahadi yangu ya muda mrefu na narudia tena mwanafunzi yeyote ambaye atafiwa na mzazi akiwa kwenye shule hizi hatafukuzwa shule, awe shule ya awali, msingi au sekondari ataendelea kusoma hadi amalize," alisema Dk. Rweikiza.

Kwenye hotuba yake, Kamishna wa Elimu, Dk. Lyambwene Mutahabwa aliipongeza shule hiyo kwa namna ambavyo imekuwa ikifanya vizuri kwenye mitihani yake ya kitaifa.

# Wauguzi wamvaa mkurugenzi fedha za sare

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAUGUZI katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wamemtaka Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Anderson Msumba, kuacha urasimu katika stahiki zao hususani kwenye fedha za sare.

Imeelezwa kuwa serikali hutoa Sh. 120,000 kwa ajili ya sare na badala yake wao wanapatiwa kitambaa chenye thamani ya Sh.30,000 hali inayolazimu kuingia gharama binafsi za kushona sare hizo.

Mwongozo wa serikali kupitia Wizara ya Afya unamtaka mkurugenzi au mwajiri kuwapatia wauguzi Sh. 120,000 kila mwaka kwa ajili ya sare au mavazi ya kazi lakini wengi wamekuwa hawafanyi hivyo na kusababisha wengi kujigharamia kinyume cha sheria.

Hayo yalibainishwa juzi na Muuguzi Mkuu wa Hospitali ya Halmashauri hiyo, Jane Mkumbo, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani yaliyofanyika kiwilaya katika viwanja vya hospitali.

Mkumbo alisema wanapopewa kitambaa na Sh.30,000 kwa ajili ya mashono haikidhi mahitaji yao kulinganisha na watakapopewa Sh.120,000 kila mwaka kwa sababu watakuwa na uwezo wa kushona sare, kupata viatu, kalamu na vitu vingine ambavyo vinahitaji. Kutokana na hali hiyo, alimwomba mkurugenzi kuliangalia hilo na kulitatua ili wasiendelee kuingilia bajeti ambazo ziko nje ya uwezo wao.

Alisema halmashauri hiyo ina wauguzi 284 wanatoa huduma katika zahanati, vituo vya afya na hospitali na kwamba muuguzi mmoja anahudumia wagonjwa 15 hadi 20 kwa siku badala ya sita hadi saba. Alisema hali hiyo imekuwa ikiwafanya kuwahudumia wagonjwa mpaka muda wa ziada bila kupewa malipo ya ziada kwa wakati.

Awali, akisoma risala mbele ya mgeni rasmi, Muuguzi wa Hospitali hiyo, Nchama Samson, alisema kabla ya maadhimisho, wamefanya shughuli mbalimbali zikiwamo kuwapima wagonjwa kifua kikuu (TB), kisukari, uzazi wa mpango, shinikizo la damu, maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU), wingi wa damu kwa wajawazito na kutoa elimu ya lishe.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Afya na Serikali Kuu (TUGHE) Mkoa wa Shinyanga, Dk. Allan Masanja, alisema malalamiko yote ya maslahi ya wafanyakazi yako katika mazungumzo na yatafanyiwa kazi kwa wakati. Alisisitiza kuwa kila mmoja atapata haki yake na kuwataka kufanya kazi kwa kuzingatia miongozo, sheria na kanuni za utumishi wa umma.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, alisema serikali imeendelea kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya afya ikiwamo ya uhaba wa watumishi na hivi karibuni ilitangaza ajira, hivyo zahanati na vituo vya afya vyenye wauguzi wachache, vitaongezewa na kutoa huduma kwa wananchi vyema.

## HABARI KITAIFA




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiangalia majiko sanifu ya umeme yanayosambazwa na Taasisi ya Tatedo kwa kushirikiana na Sescom yaliyokuwa kwenye maonyesho katika mkutano wa wadau wa nishati mjini Dodoma mwishoni mwa wiki. Kushoto kwake ni Waziri wa Nishati, Januari Makamba na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Jenista Mhagama (kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mazungumzo serikali, Shell kuhusu gesi asilia yakamilika

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema mazungumzo na kampuni ya Shell kuhusu mradi wa kuuza gesi asilia nje ya nchi na nyingine kutumika nchini, yamekamilika na sasa ni hatua ya kuanza utekelezaji.

Akizungumza jana na Nipashe kwa simu, Makamba alisema mradi huo ambao utakuwa mkubwa wa nishati barani Afrika na Tanzania una uwekezaji wa zaidi ya Dola za Marekani bilioni 42 ambazo sehemu kubwa zitatumika nchini.

"Nina furaha kwamba tumekamilisha mazungumzo ya mradi mkubwa wa nishati nchini na barani Afrika. Baada ya miaka mingi ya mazungumzo, hatimaye wamefanikiwa katika awamu hii na sasa tunakwenda kwenye utekelezaji wenye faida kwa nchi yetu," alisema.

Kuhusu manufaa ya mradi huo, Makamba alisema kuongezeka kwa fedha za kigeni, ukuaji wa pato la taifa, ajira za moja kwa moja kwa Watanzania 10,000 nyinginezo zitakazofikia 40,000. Kwa mujibu wa waziri huyo, manufaa mengine ni kuongeza uwezo na ujuzi wa Watanzania katika sekta ya mafuta na gesi, mapato ya serikali yatakayotokana na mauzo ya gesi, gawio kwa kuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ni mbia atakayepata ya mradi.

"Upatikanaji wa gesi nchini pamoja na kwamba itauzwa nje, lakini kuna kiwango ni cha matumizi ya ndani itasaidia kwenye uzalishaji wa umeme, usalama wa nishati utaongezeka," alibainisha.

Kuhusu manufaa ya moja kwa moja kwa Watanzania (local content) alisema: "Wajasiriamalia wa Watanzania watanufaika katika huduma na bidhaa zitakazohitajika katika kutekeleza mradi kuanzia usafirishaji, ujenzi wa nyumba, huduma za kifedha na ulinzi." Pia alisema katika mzungumzo kuna baadhi ya huduma wameweka mazingira zitatolewa na Watanzania usafirishaji, chakula, ujenzi wa nyumba ambazo hazihitaji mtaji mkubwa au teknolojia ambayo hatuna.

"Tumeanza maandalizi ya wajasiriamali kuzijua fursa na kujua namna ya kuzifikia, huu ni mkakati wetu kuhakikisha kila Mtanzania kwenye mnyororo wa thamani ananufaika. Kazi kubwa itafanyika kuanzia sasa ni kuelimisha umma ili tusipitwe kwa namna yoyote," alisema.

Kuhusu kushuka kwa bei ya gesi na kuachana na matumizi ya mkaa, Waziri Makamba alisema: "Bei ya gesi itakuwa nzuri na Watanzania wengi wataweza kutumia, tunahitaji kuwekeza ili iwafikie kwenye nyumba zao, kuna mpango wa kuhuisha Mpango wa Matumizi ya Gesi (National Gas Utilization Plan) ili kujua kiasi cha uwekezaji unaotakiwa ndani ya nchi."

Pia alifafanua mchango wa mradi huo kwenye Pato la Taifa kuwa ni Sh. bilioni 7 kwa mwaka, na kwamba ongezeko hilo litaleta ustawi ustawi wa Watanzania katika sekta zote muhimu na kustawisha hali zao maisha ya Watanzania.

Jana, Makamu wa Rais wa Kampuni ya Shell Jared Kuehl, alieleza furaha yake baada ya kukamilika kwa mazungumzo baina ya pande zote.

"Sambamba na kukamilika kwa mazungumzo baina yetu (Tanzania na Shell) tutasaini makubaliano ambayo yatahusisha mradi wa uchimbaji gesi asilia chini ya bahari,"alisema.

Kuehl alisema kukamilika kwa makubaliano hayo ni hatua kubwa katika kuanza utekelezaji wa mradi huo kwa kuanza na upembuzi yakinifu karibuni.

Alisema Kampuni ya Shell na Equinor kama washirika wa pamoja wamefurahi kufanya kazi kwa ushirikiano na sasa wanakwenda kwenye utekelezaji wenye tija.

Wadau wengine kwenye mradi huo ni Kampuni za ExxonMobil, MedcoEnergi, Pavilion Energy na Shirika la TPDC na serikali ya Tanzania.

Kwa mujibu wa kiongozi wa makubaliano ya mradi huo, Charles Sangweni, pia wamekubaliana kwenye usalama wa ardhi na matumizi yake.

"Tunayo furaha kuwa ni hatua kubwa ya utekelezaji wa mradi ingawa bado tuna kazi ya kufanya. Kama kila kitu kitakwenda kilivyopangwa nina uhasiri wa kusema tutafikia uamuzi wa mwisho kabisa wa uwekezaji," alisisitiza.

# Avamiwa, kujeruhiwa na fisi, ang'olewa sehemu nyeti

**Na Hamisi Nasri, LINDI**

MKAZI wa Kijiji cha Lutamba mkoani Lindi, Arafa Ibrahim, amejeruhiwa na fisi sehemu mbalimbali za mwili zikiwamo za siri akiwa amelala nyumbani kwake usiku.

Mwanamke huyo alikuwa amelala ndipo fisi huyo alipoingia na kumvamia, hivyo kumsababishia majeraha na maumivu makali. Viongozi wa kijiji hicho, wamethibitishwa kutokea kwa tukio hilo.

Ibrahim, akiwa amelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Lindi ya Sokoine, alisema jana kuwa fisi huyo aliingia ndani mwake juzi majira ya saa 5:30 usiku akiwa amelala chumbani, ndipo alipomvamia, kumshambulia na kumsababishia majeraha.

Baada ya kuvamiwa na fisi huyo, alisema alipiga yowe kuomba msaada kutoka kwa majirani ndipo alipotokea mtoto wake ambaye analala upande wa pili wa nyumba hiyo na kuanza kumsaidia.

Ibrahimu alisema fisi huyo alimvamia kijana huyo na kuanza kumjeruhi na kijana huyo kukosa uwezo wa kumsaidia mama yake ambaye alikuwa tayari ameshajeruhiwa na mnyama hiyo.

Alisema alipoona kijana wake pia anajeruhiwa, alijivuta kwenye eneo ambalo alikuwa ameweka panga ndani ya chumba chake na kujaribu kumkata fisi hiyo lakini hakufanikiwa badala yake alimkata kijana wake mkononi.

Alisema fisi huyo aliendelea kuwajeruhi yeye na kijana wake licha ya kupambana vikali na mnyama huyo kwa muda mrefu bila ya kupata msaada wowote.

Alisema baada ya kupiga kelele kwa muda mrefu kuomba msaada na wakiwa tayari katika hali mbaya kutokana na kujeruhiwa, walitokea baadhi ya majirani na kuanza kusaidia kuwanusuru.

"Kama unavyoniona hapa viganja vyote vya mikono yangu vimekatwa lakini pia nimenyofolewa sehemu zangu za siri, hivyo ndoto ya kuishi na mume haipo tena na hii inatokana na fisi kuvamia ndani mwangu na kuanza kunijeruhi vibaya mimi na kijana wangu. Hapa naomba msaada wa vyakula na mahitaji mengine ya msingi," alisema.

Ibrahimu alisema fisi huyo alipoona kundi la watu wameingia ndani kujaribu kupambana naye, ghafla alikimbia na kutoweka huku akiacha baadhi ya watu akiwa amewajeruhi vibaya sehemu mbalimbali za miili yao.

Daktari wa Upasuaji katika Hospitali ya Sokoine, Abubakar Salehe, aliyempatia matibabu baada ya kufikishwa hospitalini hapo, alisema hali yake inaendelea vyema.

Alisema alipokuwa akipokewa hospitalini hapo hali yake ilikuwa mbaya kutokana na majeraha aliyokuwa ameyapata kutokana na kujeruhiwa na mnyama huyo huku akibainisha kuwa miongoni mwa sehemu alizonyofolewa ni za siri.

Pia alisema viganja vyote viwili vimekatwa kutokana na kujeruhiwa vibaya na kwamba sehemu zake za siri zimeshonwa kwa sababu nyama kubwa ilikuwa imekatwa na kuachwa ikining'inia.


## KUPOTEA KWA CHETI



**JONATHAN EMMANUEL** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha **NNE,KOM SECONDARY SCHOOL** chenye Index No.S **2652-0107** kilichotolewa mwaka 2016 na Baraza la Mitihani Tanzania(NECTA). Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:**MAS/RB/432/2023**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
21.05.2023

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **23.05.2023** hadi **30.05.2023** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha gari tupu wenye vipimo vikubwa kutoka Mzenga kuelekea Bandari ya Dar Es Salaam, gari hilo lenye namba za usajili N**RB97300 / NRB54202 DS00TG GP / NRB 53910**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - Mita 29.5**
   **Upana - Mita 4.30**
   **Kimo - Mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **Mzenga hadi Banadari ya Dar Es Salaam kupitia Mlandizi na Morogoro road,** gari litasafiri muda wa mchana tu. ***( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

RIPOTI MAALUM

## KUYUMBA UCHUMI VIWANDA-1

# Urafiki kutoka kiwanda hadi maghala na ofisi za mabasi

## - Ukumbi burudani umegeuzwa kanisa, maeneo mengine gereji

**Na Mwandishi Wetu**




Mwonekano wa eneo lililokuwa na mitambo katika Kiwanda cha Nguo cha Urafiki ambalo limegeuzwa kuwa godauni la matrekta, vioo na bidhaa mbalimbali za wafanyabiashara kutoka nje ya nchi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

NI maumivu. Ndicho unachoweza kusema unapotembelea kiwanda cha nguo cha Urafiki kilichoanzishwa mwaka 1966 kwa ushirikiano baina ya Tanzania na China. Kiwanda hicho eneo lake yakiwamo maghorofa ya makazi, kimegeuka kuwa maghala, ofisi za watu binafsi, maegesho ya magari, gereji na vituo vya mabasi ya mikoani badala ya kuzalisha nguo na kutoa ajira kwa mamia ya Watanzania.

Kiwanda hicho ni cha kihistoria kilichoanzishwa na serikali ya Tanzania, ikiwa na hisa asilimia 49 na Jamhuri ya Watu wa China yenye asilimia 51. Baada ya kusuasua, serikali iliiomba nchi hiyo kutafuta mbia na China ilikasimu ombi hilo kwa Jimbo la Liangsu ambalo ni bingwa katika tasnia ya nguo.

Serikali hiyo iliteua kampuni ya Dieqiu Textile Dyeng (DTD) Printing Group ambayo haikufanya vizuri hadi mwaka 2017 ilipoletwa Changzhou State Owned Textile Assets Operations Limited ambayo iliahidi itapunguza hisa zake kutoka 51 na kuipatia Tanzania zaidi.

Waliokuwa wafanyakazi na waliopo sasa, wanashangazwa na kasi ya kubadili matumizi ya eneo hilo kutoka kiwanda hadi sasa maduka, ofisi na magodauni ya kuhifadhia bidhaa kutoka nje ya nchi.

Kiwandani wamebaki wafanyakazi wachache huku maeneo ya uzalishaji yakigeuzwa maghala ya kuhifadhia magari, vipuri na mizingo mbalimbali ya wafanyabiashara na wachuuzi wa bidhaa za China.

Kwenye nyumba za ghorofa zilizokuwa na zinazotumiwa na wafanyakazi, zinazotazamana na barabara ya Morogoro, sasa ni ofisi binafsi na maegesho ya magari. Pia kwenye maeneo ya wazi ya ghorofa hadi ghorofa kuna maegesho na gereji za magari huku mabasi yakiingia na kutoka kuanza au kumaliza safari za kutoka Dar es Salaam hadi mikoani na kurudi.

Nyumba wanazoishi wafanyakazi ni chakavu. Ukiangalia rangi huwezi kuitambua, kuta zimebomoka, sakafu zimefubaa. Eneo la nyuma ilikokuwa Urafiki Social Hall, kwa sasa kuna kanisa, gereji huku ziliko nyumba za maofisa wa China kuna ukuta mrefu na geti lenye walinzi muda wote.

Wafanyakazi walioko kazini wamebakisha chini ya miaka mitano kustaafu na hawazidi 150. Kadri muda unapokwisha wanalazimishwa kuhama kwenye nyumba wanazoishi na zinageuzwa ofisi kwa ajili ya ofisi za watu binafsi na kampuni.

Nipashe ilipiga kambi eneo la kiwanda na katika uchunguzi, ilibaini hakuna uwezekano wa kufufuliwa upya, labda kijengwe upya kutokana na mitambo kung'olewa muda mrefu. Baadhi ya majengo ni chakavu kiasi cha mabati kuwa chekecheke na kasi ya kugeuza matumizi ya eneo ili kupata kipato ikiongezeka siku hadi siku.

### CHAMA CHA WAFANYAKAZI

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Huduma na Ushauri (TUICO) Tawi la Urafiki, Saidi Mteje, anasema: "Nimekuwapo kiwandani tangu mwaka 1982 nimeshuhudia mengi kutoka mzunguko mmoja wa wafanyakazi 5,000 hadi 6,000 kwa saa 24 na sasa tuko 150 na hatuna kazi za kufanya zaidi ya kufanya usafi, kuripoti kwamba tupo na kuondoka."

Anasema enzi Rais Benjamini Mkapa wakati Waziri wa Viwanda na Biashara akiwa Dk. Abdallah Kigoda (Marehemu), kiwanda kilianza kusuasua ndipo walipoamua kukibinafsisha mwaka 1997 kwa mbia kampuni ya China, ikiwa na hisa asilimia 51 na Tanzania asilimia 49.

"Naweza kusema walipoingia mkataba hawakuangalia umuhimu wa maisha ya Mtanzania. Walichoangalia ni mapato ya kodi lakini athari hawakuiangalia. Walipoanza kazi wakaanza kupunguza wafanyakazi, mzunguko haukuwapo. Waliondolewa wafanyakazi 800 kwa wakati mmoja. Watu walikosa kazi, mishahara ikaanza kuchelewa na kuna wakati tulikaa nyumbani mwaka mmoja kupisha matengenezo ambayo hayakufanyika," anasema.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, alikuwa analipwa Sh. 60,000 kwa mwezi na kwamba mamlaka ya utawala alikabidhiwa Mtanzania lakini mambo ya fedha, uwekezaji na mengine walisimama wenyewe (wawekezaji) na ndio walikuwa na sauti kubwa.

"Hata mali za kampuni walikabidhiwa zikiwamo majengo na maeneo yote ya kiwanda. Ghafla tuliona mabadiliko makubwa kama kung'oa mashine za mwanzo kwa madai wataleta nyingine lakini hawakuleta na sehemu zikabaki wazi, wakaleta nyingine wakazifunga kwingine. Ni hujuma kubwa kwa kiwanda na nchi yetu," anasema.

Kwa mujibu wa Mteje, kiwanda hicho kilikuwa kimoja ndani ya vitano. Kulikuwa na sehemu ya nyuzi, kufuma, uchapaji wa nguo kama kanga, vitenge, mashuka na sare za jeshi.

### MITAMBO YANG'OLEWA

"Waling'oa mitambo na kuleta mingine ya ufumaji, huku eneo la nyuzi palifungwa na wafanyakazi wakapunguzwa. Uzalishaji ukawa wa upande mmoja kwamba, kitambaa kinachukuliwa kinapelekwa kwingine (China) kwa ajili ya kuchapwa na kutengeneza nguo," anasema.

Kiongozi huyo anasema mashine zilizokuwa eneo la uchapaji, ziling'olewa na hawajui zilikwenda wapi lakini waliona vitambaa vikiletwa kwa ajili ya kuchapwa huku ubora ukiwa siyo ule wa Urafiki.

"Vitambaa vililetwa kutoka nje kwa gharama za huko, ajira za Watanzania ziliendelea kupungua. Ilifika wakati ukihitaji kitu hata kama unaweza kukinunua Manzese, wanaagiza China kwa gharama kubwa. Nakumbuka waliagiza nati ambazo walijaribu kufunga ikashindikana hadi leo ziko stoo zimeota kutu," anasema.

### MAJI YA KISIMA

Pia anasema viliingizwa vipuri vingi kutoka nje ambavyo havikufaa. Mashine zilizofungwa zilifanya kazi kwa muda mfupi zikafa na mbaya zaidi waliacha kutumia maji ya iliyokuwa Mamlaka ya Maji Mijini (NUWA) (sasa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam - DAWASA) ambayo hayana chumvi na kuchimba kisima ndani ya kiwanda yaliyokuwa na chumvi.

"Mashine zinazochapa kanga na nguo nyingine zikaanza kutumia maji ya chumvi zikaanza kuoza taratibu, hali ilivyozidi kwenda mrama, wakaanza kuondoka mmoja mwishowe tukaona amebaki Mchina mmoja. Walikaa kwa muda wakarudi, wanaangalia kiwanda wanaondoka.

"Wakati huo baadhi ya Watanzania ndio wanawapa taarifa na haturuhusiwi kufanya lolote. Kiongozi mmoja wa serikali yetu alituambia Watanzania ni wasumbufu tuwaache wageni wanajua kila kitu," anasema.

Kwa mujibu wa Mteje, ilipofika mwaka 2016, mitambo ilikufa na ukawa mwisho wa uzalishaji. Wafanyakazi walipewa likizo kupisha ukarabati na baada ya likizo kwisha, hawakuona ukarabati uliofanyika, huku wageni hawaonekani bila taarifa yoyote.

"Mwaka 2016 serikali ilileta kiongozi kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara kusimamia kiwanda, akaanza kufanya mabadiliko lakini palitokea mgogoro mkubwa. Kila taarifa tuliifikisha kwa serikali ila majibu yao ni kwamba shughuli zinaendelea wanafanya mawasiliano na China. Tunajiuliza maswali mengi sana bila majibu," anasema.

Wakati hali ikiwa hivi, Nipashe imemtafuta Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, tangu Machi 22, mwaka huu, kwa kupeleka maswali kupitia Ofisi ya Habari ambayo hayajajibiwa.

Pia ilimtafuta Msemaji wa Serikali na Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo, Gerson Msigwa, na kumtumia maswali husika naye aligonga mwamba kupata ufafanuzi wa kinachoendelea.

ITAENDELEA KESHO




Mafundi ujenzi wakitandaza lami katika barabara ya juu Mataa ya Chang'ombe jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wanahisa CRDB waidhinisha gawio bil. 117.5/-

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MKUTANO Mkuu wa 28 wa mwaka wa wanahisa wa Benki ya CRDB, umeidhinisha mapendekezo ya Bodi ya Wakurugenzi ya benki hiyo kulipa gawio la Sh. 45 kwa kila hisa, hivyo kufanya jumla ya gawio kwa mwaka wa fedha 2022 kuwa Sh. bilioni 117.5.

Akizungumza katika mkutano huo uliofanyika Kituo cha Kimataifa wa Mikutano Arusha (AICC) huku wengine wakifuatilia ajenda zilizojadiliwa kwa njia ya mtandao juzi, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya CRDB, Dk. Ally Laay, alisema gawio lililopitishwa ni sawa na ongezeko la asilimia 25 kulinganisha na gawio la Sh. 36 kwa hisa lililolipwa mwaka jana.

Ongezeko hilo lina maana ya kuwapo uendelevu wa kuimarika kwa pato la hisa ambalo mwaka 2022 limefika Sh. 134.5. "Kwa mara nyingine tena, tunafurahi kupata matokeo mazuri kwa mwaka 2022 yaliyochangia kuongeza thamani kwa wanahisa wetu.

"Faida tuliyoipata mwaka 2022 ni uthibitisho wa utekelezaji makini wa mpango mkakati wetu wa miaka mitano wa 2018 - 2022. Benki ilipata faida ya baada ya kodi ya Sh. bilioni 351.4 sawa na ongezeko la asilimia 31 kulinganishwa na Sh. bilioni 268.2 za mwaka 2021," alisema Dk. Laay.

Vilevile, Dk. Laay alisema kampuni tanzu ya Burundi nayo inazidi kuimarika, hivyo kuwa na mchango mkubwa zaidi kwenye faida ya kampuni mama.

Alibainisha kuwa kwa mwaka 2022, Benki ya CRDB Burundi imepata faida kubwa zaidi tangu ilipoanzishwa mwaka 2012. Kampuni hiyo tanzu ilipata faida ya Sh. bilioni 23 mwaka 2022 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 79.7 kutoka Sh. bilioni 12.8 iliyopatikana mwaka 2021. Kwa faida hiyo, kampuni tanzu hiyo ilichangia asilimia saba katika faida ya kampuni nzima.

"Nina furaha kuwataarifu kwamba hivi karibuni tumepata leseni ya kuanza kutoa huduma za fedha kutoka Benki Kuu ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (BCC).

"Vilevile, benki yetu imeanzisha kampuni tanzu mbili mwaka huu ambazo ni CRDB Bank Foundation na CRDB Insurance Company ikiwa ni benki ya kwanza kuanzisha kampuni tanzu kamili ya bima nchini," alisema Dk. Laay.

Akizungumzia utendaji wa benki, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema kuwa kwa mwaka wa fedha 2022, waliendeleza juhudi za kukuza mapato na wakafanikiwa kwa kiasi kizuri.

Alibainisha kuwa mapato ya uendeshaji yaliongezeka kwa asilimia 28 na kufika Sh. bilioni 745.8, yakichangiwa na kuongezeka kwa mikopo iliyotolewa. Kwa mwaka 2022, uwiano wa mikopo chechefu ulishuka mpaka asilimia 2.8, hivyo kuwa ndani ya ukomo uliowekwa kikanuni na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) wa kutozidi asilimia tano.

Nsekela alisema mizania ya benki pia ilikua kwa asilimia 32 kutoka Sh. trilioni 8.8 mwaka 2021 mpaka Sh. trilioni 11.6, hivyo kuwa taasisi ya kwanza ya fedha nchini kuvuka Sh. trilioni 10.

Mkurugenzi huyo alisema ongezeko hilo limechangiwa na kuimarika kwa amana za wateja zilizoongezeka kwa asilimia 26.4 na kufika Sh. trilioni 8.2 kutoka Sh. trilioni 6.5 za mwaka 2021.

"Juhudi zetu za kuimarisha huduma zetu zilituletea mafanikio hasa katika kubana matumizi kwani uwiano wa gharama na mapato uliimarika kutoka asilimia 66.7 mwaka 2018 mpaka asilimia 49.4 mwaka 2022," alisema Nsekela.

Nsekela alisema ufanisi uliopatikana umewezesha kuwekeza zaidi kuimarisha huduma kwa kuwekeza kwenye majukwaa ya kidijitali ambayo yanasaidia kukidhi mahitaji ya wateja kwa kuwapa huduma wazitakazo mahali walipo na kuzitumia kwa namna waitakayo.

"Leo hii zaidi ya asilimia 95 ya miamala yote ya benki inafanyika kidijiti, hasa kupitia SimBanking, huduma za benki kwa intaneti na kwa zaidi ya mawakala 28,000 wa Benki ya CRDB," alifafanua.

Nsekela alisema kuwa katika miaka mitano iliyopita, benki ilianzisha ubia wa kimkakati ambao umechangia katika mafanikio yake kwa mwaka 2022.

Katika kipindi hicho, ubia huo umeiwezesha Benki ya CRDB pamoja na kampuni zake tanzu kukuza mtaji, kuwa na teknolojia ya kisasa na kuboresha huduma, hivyo kukidhi matarajio ya wateja.

Kuhusu mikakati ya baadaye, Nsekela alisema Bodi ya Wakurugenzi imeidhinisha mpango mkakati wa miaka mitano kuanzia mwaka 2023 - 2027 unaosisitiza kujenga uchumi shirikishi, kuongeza thamani endelevu kwa wanahisa na kuingia katika ubia wa kimkakati ili kuikuza benki na kuongeza ushawishi wake sokoni.

Alisema mpango mkakati huo umetanguliza mbele maslahi ya wateja, jambo lenye maana kwamba benki sasa inawekeza katika kuyatambua mahitaji ya wateja na kuyafanyia kazi ili kukidhi matarajio yao.

Nsekela aliwashukuru wanahisa wa benki hiyo kwa ushirikiano ambao wameendelea kuipatia menejimenti na wafanyakazi wa benki hiyo na kuwahakikishia benki itaendelea kufanya vizuri ili kuwapa thamani ya uwekezaji walioufanya na wanaoendelea kuufanya.

Akizungumzia gawio lililoidhinishwa, Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Benki ya CRDB ambaye kwa sasa ni Mbunge wa Vunjo, Dk. Charles Kimei, alisema wanahisa wamefurahia ongezeko la gawio lililopendekezwa.

Dk. Kimei aliongezea kuwa kitendo cha CRDB kutoa gawio kiila mwaka kimekuwa kikiwavutia wawekezaji wengi ndani na nje ya nchi kuwekeza katika hisa za benki hiyo.

# Ufaransa yafungua milango utalii Tanzania

**Na Daniel Sabuni,** HAI

BODI ya Utalii Tanzania (TTB), imesema hali ya utalii nchini inaendelea kuchanua siku hadi siku baada ya Ufaransa kufungua milango kwa kuruhusu raia wake 207 kuitembelea Tanzania.

Ujio huo ni wiki moja tangu kuwasili nchini kundi lingine la mawakala 40 wa utalii kutoka nchini China.

Akizungumza jana katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), Kaimu Mkurugenzi wa Masoko wa TTB, Dk. Gladstone Mlay, alisema kwa sasa Tanzania inandelea kupokea makundi ya watalii kutoka mataifa mbalimbali duniani, ikiwa ni sehemu ya kutimiza malengo ya serikali ya kufikisha watalii milioni tano, ifikapo mwaka 2025.

"Hawa Wafaransa waliowasili nchini, ni moja ya malengo ya kimkakati ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kufikisha watalii milioni moja kutoka katika taifa hilo kubwa na lenye nguvu kiuchumi, ambao wataitembelea Tanzania. Mwaka jana peke yake, watalii 100,370 kutoka nchini humo waliitembelea Tanzania.

"Utaona katika kanzidata yetu watalii kutoka Marekani kwa mwaka jana ambao waliitembelea Tanzania walikuwa 160,000. Kwa hiyo taifa linalofuatia kwa kuleta watalii wengi zaidi ni Wafaransa. "Tunachotaka hivi sasa ni kuhakikisha watalii hawa wanaongezeka, lakini kupata wageni kutoka mataifa mengine makubwa duniani na yenye nguvu kiuchumi ili kuitangza Tanzania kimataifa," alisema.

Baada ya mapokezi hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Usimamizi na Uendeshaji wa KIA, Christina Mwakatobe, alisema wamejipanga kuhakikisha watalii wanaposhuka, wanapata huduma nzuri kabla hawajaenda kutembelea hifadhi za taifa, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na vivutio mbalimbali vya utalii vilivyoko Kaskazini mwa Tanzania.

"Huduma nzuri inaanzia hapa uwanjani tu wanaposhuka kuhakikisha tunawapokea vizuri, tunawahudumia kwa haraka na tumeweka ngoma ya asili ambayo nyie wenyewe mmejionea kila mgeni alivyofurahia na kuanza kurekodi," alisema Mwakatobe.

Kwa mujibu wa Mwakatobe, wiki mbili zilizopita, uwanja huo ulipokea watalii zaidi ya 250 kutoka Ubelgiji, ambao kimsingi ni matunda ya filamu ya The Royal Tour, inayotangaza uzuri wa hifadhi na vivutio vya utalii Tanzania.

Wilbert Mbise, mwongoza watalii na mwenyeji wa wageni hao, alisema watahakikisha kila mgeni anayekuja anatamani kurudi tena Tanzania kulingana na huduma watakazowapatia.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga inastahili pongezi, si kubezwa

**WIKI** iliyopita tumeshuhudia historia nchini katika anga la michezo hususani mchezo wa mpira wa miguu ikiandikwa baada ya mabingwa wa soka Tanzania, Yanga kufanikiwa kutinga kwa kishindo hatua ya fainali ya kombe la Shirikisho Afrika.

Yanga iliwashangaza wengi Afrika baada ya kuifunga nyumbani (2-0) na ugenini (2-1) Marumo Gallants ya Afrika Kusini na kukata tiketi ya kucheza hatua hiyo ya mwisho dhidi ya USM Alger ya Algeria.

Kwa hapa nyumbani kama ilivyo kawaida ya ubishani na upinzani wa 'U-Simba na U-Yanga' wapo walioingia kwenye mtego wa kubeza juhudi za Yanga kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania kwenye michuano hiyo namba mbili kwa ukubwa barani Afrika.

Kiuhalisia mpaka Yanga inafika kwenye hatua hii ya fainali, imekutana na vigogo wengine wa soka katika nchi tofauti, kubeza kuwa Yanga imekutana na timu dhaifu kwenye safari yake kuelekea hatua ya fainali si sababu za 'kiuwanamichezo' hata kidogo.

Kwenye michuano mikubwa kama hii kuanzia hatua ya makundi hakuna timu nyepesi isipokuwa kuna kuzidiana kwa mbinu na maarifa katika kila mchezo.

Wapo wanaosema Yanga si timu ya kwanza Tanzania kufika hatua hiyo ya fainali ya michuano ya kombe la Shirikisho wengi wakitaja Simba kufikia hatua hiyo mwaka 1993.

Ni kweli Simba walifika hatua hiyo wakati huo michuano hiyo ikiitwa kombe CAF kabla ya kuunganishwa na kombe la Washindi Afrika na kuzaliwa michuano ya kombe la Shirikisho Afrika.

Pamoja na hayo yote, tangu mwaka huo wa 1993 ambao Simba alitinga hatua ya fainali kombe la CAF mpaka sasa ikiwa ni miaka 30, hakuna timu iliyokuwa imetinga hata hatua ya nusu fainali tu ya michuano inayoandaliwa na CAF.

Kwa Yanga kufika tu hatua ya nusu fainali ya kombe la Shirikisho ilikuwa hatua kubwa kwa vilabu vyetu tangu miaka 30 iliyopita, kutinga hatua ya fainali ni hatua kubwa zaidi ambayo Yanga imeipiga na soka la Tanzania kwa ujumla, wanastahili pongezi. Kila timu iliyoshiriki katika michuano hii ilikuwa na lengo la kufanya vizuri ikiwezekana kufika fainali na kuchukua ubingwa, lakini kutokana na ushindani uliopo timu zote zimeshindwa kufika hatua ya fainali isipokuwa kwa Yanga na wapinzani wao katika hatua hiyo klabu ya USM Alger ya Algeria.

Yanga hakika wanastahili pongezi kwa kupeperusha vyema bendera ya Tanzania kwenye michuano hiyo ya Shirikisho na imetangaza jina la Tanzania kwenye medali ya soka.

Na ndio maana si ajabu kuona Rais wetu mpendwa, Samia Suluhu Hassan akishawishika kutoa ndege ya serikali kuwapeleka Yanga Algeria kwenye mchezo wao wa marudiano huku pia akitoa ahadi ya Sh. milioni 20 kwa kila goli katika mechi watakayoibuka na ushindi.

Wito wetu Watanzania, Yanga wanapaswa kujiandaa vyema kuelekea kwenye mchezo wa fainali na wajiwekee lengo la nini wanataka katika kila mchezo wa fainali.


Ipo wazi Yanga watacheza michezo miwili ya fainali, kwa maana ya nyumbani na ugenini, michezo hii ni ya matokeo zaidi, hivyo benchi la ufundi na wachezaji wa Yanga lazima wajipange vizuri katika kila mchezo.

Yanga, ambao tayari wametangazwa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/2023, wataanzia nyumbani Mei 28 kwenye mchezo wa fainali ya kwanza kabla ya kuwafuata 'Waarabu' Juni 3.

Ni vizuri kwa Yanga kumaliza kazi nyumbani kwa kuhakikisha wanapata ushindi mnono ili kurahisisha kazi kwenye mchezo wao wa marudiano jijini Alger, Algeria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Ni tuzo ya kiungo bora wa msimu na si ya mechi moja

**BAADA** ya Kamati ya Tuzo za Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), juzi kutangaza majina ya wachezaji, makocha na waamuzi, watakaowania tuzo mbalimbali baada ya kufanya vizuri kwenye msimu wa Ligi Kuu 2022/23, tayari kama kawaida maoni kutoka kwa wadau mbalimbali yameanza kusikika kutolewa.

Mengine ya kupongeza na mengine ya kukosoa. Haikatazwi kwa sababu soka ndiyo mchezo ambao una demokrasia zaidi kuliko kitu kingine chochote.

Soka ndiyo mchezo ambao hata kocha ambaye ni mtaalamu anaweza kupondwa na mashabiki, yaani wao ndiyo wanajua zaidi kuliko kocha.

Wao ndiyo wanataka kupanga wachezaji, wanaweza kukupangia viungo washambuliaji zaidi ya watano kwenye mechi moja, bila kuangalia wachezaji muhimu wakati timu ikiwa haina mpira.

Baadhi ya mashabiki wanachotaka ni kuona chenga, kanzu, matobo, pasi nyingi zisizo na maana na mabao tu, hilo ndilo soka.

Baada ya majina ya wawania tuzo kutolewa, tayari wameanza kujitokeza watu ambao wanakosoa uteuzi wa wawania tuzo hizo, wengi wanaonekana hawakubaliani na kipengele cha kiungo bora wa msimu.

Walioteuliwa kuwania tuzo ya kiungo bora ambayo imeibua minong'ono mingi ni Bruno Gomes wa Singida Big Stars, Mzamiru Yassin wa Simba, Stephane Aziz Ki wa Yanga, Clatous Chama wa Simba na Saido Ntibazonkiza, akizichezea klabu mbili kwa nyakati tofauti, Geita Gold na Simba.

Wachezaji hawa watano ndiyo walioteuliwa kuwania tuzo ya msimu, kipengele ambacho ndicho kinalalamikiwa na wengi.

Wanaolalamika wanadhani kuwa wapo wachezaji wengine kwenye nafasi hiyo ambao wangepaswa kuwepo.

Baadhi ya wachezaji wanaotajwa kustahili kuwamo kwenye kipengele hicho lakini hawamo ni Khalid Aucho wa Yanga, James Akaminko na Sospeter Bajana wa Azam FC.

Wapo walioenda mbali na kumtaja Yannick Bangala pia kuwa alistahili kuwamo kwenye kinyang'anyiro hicho.

Binafsi nakubaliana na wote ambao wamewataja kina Bangala, Aucho, Akaminko na Bajana kuwa ni moja ya viungo bora sana kwenye ligi yetu nchini kwa sasa. Lakini niungane tu na Kamati ya Tuzo kuwa haikufanya makosa yoyote kuwateua iliyowateua na kuwaacha iliyowaacha.

Kwangu mimi walioteuliwa wote wamestahili na yoyote kati yao akipata, atakuwa anastahili kwa sababu ni lazima mshindi awe mmoja.

Ukiangalia wachezaji kina Bruno, Mzamiru, Aziz Ki, Chama na Saido wamekuwa kwenye viwango vya hali ya juu kwenye mechi nyingi, au tuseme msimu mzima.

Viungo kama Chama, Bruno na Saido wanabebwa na namba na takwimu, huku wengine viwango walivionyesha.

Huwezi ukawaacha Chama, Saido na Bruno, na kuwaweka kina Akaminko ambao wanabebwa na kucheza vizuri kwenye mechi moja au zisizozidi nne .

Hizi ni tuzo za kiungo bora wa msimu na si za kiungo bora wa baadhi ya mechi fulani fulani, na hili walizingatie zaidi hata kuelekea kwenye msimu ujao wa ligi.

Bajana na Akaminko, mara nyingi tunawaona wanafanya kazi nzuri sana timu yao ya Azam FC inapocheza dhidi ya vigogo, Simba na Yanga, katika mechi hizo wanaonyesha kujituma zaidi na kuonyesha kiwango kikubwa.

Ifike sehemu wachezaji wetu waache kukamia mechi moja, badala yake kucheza vizuri mechi zote.

Simba na Yanga, wachezaji wao wanalazimika kucheza vizuri kila mechi, hata wakicheza na timu ndogo kutokana na presha ya mashabiki wao, ndiyo maana mara nyingi huingia wengi kwenye tuzo hizi.

Ukiona mchezaji hachezi vizuri Simba au Yanga, basi ujue kiwango chake kimeshuka kwa sababu wao ndiyo huwa wanakamiwa na si kukamia.

Mimi nadhani Kamati ya Tuzo ipo sahihi na hili ni somo kwa wachezaji wote kuwa wanatakiwa wacheze mechi zote kwa usawa na si kuchagua baadhi ya mechi.

Nimpongeze Mbrazil Bruno, huyu anacheza vizuri kwa kiwango kile kile kwenye mechi zote. Hachagui mechi za maonyesho ili watu wamuone, hucheza kwa manufaa ya timu na ndiyo maana wala si ajali wala upendeleo kuingia kwenye tuzo hizo na haitokuwa ajabu akashinda.

Wachezaji wa Ligi Kuu, husasani wazawa wanapaswa kumwiga huyu nyota wa Brazil.

# WMA yatia mkono kukomesha vipimo batili

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Vipimo (WMA) imeadhimisha Siku ya Vipimo Duniani Mkoa wa Kigoma kwa kugawa seti 25 za vipimo zenye ujazo wa lita tano, lita 10 na 20 kwa lengo la kuhimiza matumizi ya vipimo sahihi wakati wa uuzaji na ununuzi wa mawese.

WMA ilitoa seti hizo za vipimo ili kuwawezesha wafanyabiashara hao kuachana na matumizi ya vipimo batili, maarufu kama bidoo, ambayo huwanyonya na kuwapunja wakulima wakati wa mauzo.

Maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani huadhimishwa kila mwaka ifikapo Mei 20 na kauli kaulimbiu ya maadhimisho haya kwa mwaka 2023 ilikuwa "Vipimo Katika Kuwezesha Mfumo wa Usambazaji wa Chakula Duniani".

Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stella Kahwa, ndiye aliyegawa seti za vipimo hivyo kwa vikundi 24 vya wakulima na aliziomba halmashauri za mkoa wa Kigoma kutenga fedha na kununua vipimo vingine ili kuwasaidia wakulima.

Alisema vipimo vitawasaidia wakulima kuuza mawese kwa kutumia vipimo sahihi na kutekeleza kampeni ya kutokomeza matumizi ya vipimo batili inayosema "bidoo sasa basi".

Kahwa alisema jukumu la kusimamia haki katika biashara ambalo lipo katika Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara linatekelezwa na Wakala wa Vipimo ikiwa ni taasisi mwanachama wa Shirika la Vipimo Duniani (OIML).

Alisema shirika hilo hutoa miongozo mbalimbali kuhusu vipimo baada ya kufanya tafiti za kisayansi.

Mwaka 1875, alisema nchi mbalimbali zilikutana Ufaransa na kwa pamoja zilikubaliana kipimo kitachotumika katika nchi moja kiwe sawa sawa na kipimo kitachotumika katika nchi zingine.

"Ndiyo maana hata vipimo tulivyoleta na kukabidhi kwenye maadhimisho haya vina usahihi wa hali ya juu na vimewekewa alama maalumu uhakiki ambayo ni muhuri wa bibi na bwana," alisema.

Naye Kanali Isack Mwakisu, Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa, Thobias Andengenye, aliupongeza uongozi wa WMA kwa kuchagua kufanya maadhimisho kitaifa kwenye Mkoa wa Kigoma na kwa kuona umuhimu wa kutengeneza vipimo seti 25.

Alisema vipimo hivyo vilivyogawiwa kwenye vikundi mbalimbali vya wakulima kwa ajili ya kuhimiza matumizi sahihi ya vipimo na kuachana na batili maarufu kama bidoo vitakuwa msaada mkubwa kwa wakulima.

Kanali Mwakisu alisema vipimo vinatumika kwa namna mbalimbali kwenye maisha ya kila siku na katika shughuli za kilimo vipimo hutumika kuanzia uandaaji wa shamba, kupanda mbegu, umwagiliaji, uwekaji wa mbolea shambani hadi wakati wa uvunaji na usambazaji wa mazao.

Alisema vipimo ni nyenzo muhimu ambayo hutumika wakati wa kuuza hata wakati wa kusafirisha mazao kutoka sehemu moja hadi nyingine hivyo, wakulima wote wanapaswa kuzingatia matumizi sahihi ya vipimo kwenye mfumo mzima wa uzalishaji na usambazaji wa chakula.

Amina Mohamed, mkulima na muuzaji wa mawese Wilaya ya Buhigwe, alisema vipimo walivyopatiwa vitawasaidia kuuza mawese kwa kutumia vipimo sahihi.

Alisema hawatatumia tena ndoo kwani wanunuzi walikuwa wanawapunja kwa kutaka kujaziwa mawese kwenye ndoo kwa ujazo wa hadi kufikia kumwagika kitendo ambacho kilikuwa kinawasababishia hasara kubwa na kumnufaisha mnunuzi.



Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaazi, Mhandisi Anthony Sanga, akibadilishana hati ya makubaliano ya ushirikiano katika sekta ya ardhi na Dk. Mngereza Mzee Miraji, ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar wakati wa hafla fupi jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wizara Ardhi Muungano, SMZ zatiliana saini ushirikiano katika sekta na makazi

**Na Munir Shemweta**, DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na ile ya Makazi Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na la Zanzibar (ZHC) zimetia saini hati ya makubaliano ya ushirikiano katika sekta za ardhi na nyumba.

Hatua hiyo ni moja ya utekelezaji wa mwongozo wa ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar kuhusu taasisi zisizo za muungano kukutana na kubadilishana uzoefu wa utendaji wa majukumu yao na namna ya kukabiliana na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yao. Utoaji saini makubaliano hayo ya pande hizo ulifanywa na Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Anthony Sanga, na yule wa Makazi Zanzibar, Dk. Mngereza Mzee Miraji. NHC ikiwakilishwa na Mkurugenzi Mkuu, Hamad Abdalah na ZHC Mwanaisha Ali Said, mbele ya mawaziri wa wizara, Dk. Angeline Mabula na Rahma Kassim Ali

Maeneo yatakayotekelezwa katika ushirikiano huo ni kukusanya, kuchakata na kubadilishana taarifa za ardhi baharini, kubadilishana uzoefu kwenye maendeleo na matumizi ya mifumo ya habari na teknolojia kwa sekta ya ardhi pamoja na kuandaa na kutekeleza sera, sheria na miongozo mbalimbali ya sekta ya ardhi.

Maeneo mengine ni kushirikiana kitaalamu na kubadilishana uzoefu katika mfumo wa usimamizi na maendeleo ya sekta ya milki kuu inayojumuisha makazi na nyumba, utafiti na maendeleo kwenye sekta ya ardhi, utatuzi wa migogoro ya ardhi pamoja na ushirikiano na kubadilishana uzoefu katika usimamizi na maendeleo ya mji Mkongwe.

Akizungumza katika hafla fupi ya utiaji saini iliyofanyika juzi jijini Dodoma, Dk. Mabula alisema, makubaliano yaliyofikiwa yaingie katika utekelezaji na yawe fursa kwa kila mmoja kuona namna ya kuboresha uhusiano katika sekta ya ardhi kwa kuwa upande wa Tanzania Bara sekta hiyo ni wezeshi na inapofanya vibaya inakwaza sekta zingine.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, changamoto anayoina ni kuwa makubaliano hayo yamechelewa sana kutokana na kila upande kuwa na mambo mazuri iliyofanya na kusisitiza ushirikiano huo utakuwa njia bora za kutatua migogoro lakini kuleta salama ya milki, ufanisi na kikubwa kuona namna ya kuisimamia sekta ya ardhi.


"Msisitizo wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ni sekta ya ardhi kuwa kinara katika kuongoza na kuifanya ardhi kupangika vizuri na kuleta manufaa kwa wananchi. Sekta hii inaleta maisha bora na hatuwezi kuwa na maisha bora wakati kila siku kuna migogoro na hatuwezi kutoa fursa watu wawekeze," alisema.

Alitaka makubaliano yaliyofikiwa yasimamiwe kwa vitendo sambamba na kuwa na vikao vya mara kwa mara vya ufuatiliaji na tathmini katika kutekeleza makubalinao na kutoa rai kwa makatibu wakuu kuhakikisha makubaliano yaliyofikiwa yanatekelezwa kwa kuwekewa utaratibu mahsusi na kusimamiwa kwa kuwa na vikao vya mara kwa mara ili kujua kinachoendelea.

Waziri Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar, Rahma Kassim Ali, alisema katika utekelezaji wa makubainao hayo, kuna haja kwa wataalamu kuweka mpango kazi utakaoainisha vitu vya kuanza navyo na iwapo zipo changamoto basi ziwasilishwe kwa mawaziri kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Alisema makubaliano yaliyotiwa saini yakifanikishwa, serikali zote mbili zitakuwa zimepiga hatua kubwa na kuwafanya viongozi wake kuwa salama kwa kuwa wizara hizo zinahudumia na kutoa huduma bora kwa wananchi.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# TAKUKURU yabaini upungufu utekelezaji miradi maendeleo

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Ruvuma, imebaini upungufu katika utekelezaji wa miradi mitano ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 5.5.

Akitoa juzi taarifa ya utendaji kazi wa TAKUKURU mkoa katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Machi, mwaka huu, Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma, Janeth Haule, alisema hatua mbalimbali zilichukuliwa ili kuondoa upungufu huo kwenye miradi hiyo.

Hata hivyo, alisema katika kipindi hicho, TAKUKURU ilifuatilia utekelezaji wa miradi 15 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 6.5.

Aliitaja miradi iliyobainika kuwa na upungufu kuwa ni ujenzi wa madarasa tisa katika Shule ya Sekondari Sasawala wilayani Namtumbo wenye thamani ya Sh. milioni 180. Katika mradi huo, alisema TAKUKURU ilibaini mradi kuchelewa kukamilika kutokana na ucheleweshaji wa ununuzi wa vifaa na mafundi.

"TAKUKURU tulitoa ushauri kwa halmashauri kutoa ukomo wa bei kwa wazabuni na kufanya malipo kwa wakati baada ya kujiridhisha na uchunguzi," alisisitiza Haule.

Aliutaja mradi mwingine kuwa ni ujenzi wa majengo matatu katika Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo unaogharimu Sh. milioni 800. Katika mradi huo alisema walibaini kuchelewa kukamilika na TAKUKURU ilishauri kufanya tathmini sahihi ya vifaa na kufanya ununuzi wa jumla.

Haule aliutaja mradi mwingine waliobaini upungufu ni ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Ruvuma mjini Songea unaogharimu Sh. bilioni 3.87, alisema TAKUKURU ilibaini kuchelewa kukamilika kwa mradi, ucheleweshaji wa makabidhiano na mradi kufanyika kwa awamu mbili.

Alisema TAKUKURU ilishauri kukamilishwa haraka kwa mradi huo katika awamu ya pili ili kuepuka upotevu wa vifaa vya ujenzi kutokana na kurudia kazi moja mara mbili.

Miradi mingine iliyogundulika kuwa na upungufu ni ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbinga unaogharimu Sh. milioni 500 na ujenzi wa Kituo cha Afya cha Mbangamao Wilaya ya Mbinga unaogharimu Sh. milioni 250.

Naibu Mkuu huyo alisema katika kipindi hicho, TAKUKURU ilipokea malalamiko 20 kati ya hayo, tisa ni ya rushwa na kwamba taasisi ilitoa elimu kupitia semina 26, klabu za wapinga rushwa 70 za shule za msingi na sekondari, mikutano ya hadhara 11,vipindi vya redio vinne, Makala saba na maonesho saba.



Ofisa Raslimali Watu katika mgodi wa Barrick North Mara, Innocent Kishobera, akiongea na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Iringa wakati wa kongamano la kuwajengea uwezo lililoandaliwa na Taasisi ya AIESEC Tanzania kwa udhamini wa kampuni ya Barrick na kufanyika chuoni hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni yazindua ripoti hali ya soko EAC

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI inayojihusisha na usimamizi wa shughuli za kisheria katika nchi za Afrika ya Mashariki (ALP East Africa), imezindua ripoti inayohusu taarifa za Soko la Pamoja la Afrika Mashariki kuangazia huduma na bidhaa.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa ripoti hiyo iliyofanyika mwishoni mwa wiki Dar es Salaam, Mkuu wa ALP East Africa, Francis Gimara, alisema lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ni mwingiliano wa ushirikiano wa kiuchumi na kibiashara, ambalo ni la msingi katika mchakato wa ushirikiano.

Gimara alisema mwingiliano ya kibiashara ni msingi wa mkataba na itifaki za Umoja wa Soko la Pamoja na Forodha na unatarajiwa kuwa mhimili mkuu wa nchi wanachama wa EAC.

"Tukiwa kama watoa huduma zenye maingiliano na ushauri wa kitaalamu wa kampuni za kisheria kwenye nchi za Uganda, Kenya, Tanzania na Sudani ya Kusini, ALP ni kampuni inayotoa huduma za kisheria na ushauri kwenye nchi hizi kwa upande wa biashara pamoja na kuanzisha biashara mpya na usimamizi wake," alisema. Gimara aliongeza kuwa msaada wa kiushauri kuhusiana na biashara pamoja shughuli za kibiashara baina ya nchi moja na nyingine ni eneo ambalo ALP inalishughulikia mara kwa mara husussani kupitia sheria na taratibu za kiudhibiti za nchi wanachama wa EAC.

Alisisitiza kuwa ALP East Africa inazingatia upitiaji wa huduma za soko la pamoja la Afrika Mashariki na kutoa uelewa wa uhusiano kati ya mifumo ya udhibiti wa kitaifa na mfumo wa biashara wa kikanda. "ALP East Africa inaelewa umuhimu wa wadau katika maeneo ya biashara–katika maoni ya umma, serikali za EAC ikiwa ni pamoja na watendaji wao mbalimbali na wa ngazi tofauti) na, kwa mtazamo binafsi, watendaji wa sekta binafsi (wawekezaji, jumuiya ya wafanyabiashara, na kadhalika," alisema Gimara.

Alisema kampuni hiyo ilitoa ripoti ya Soko la Pamoja la Huduma na Bidhaa za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC CSG Scan) 2022 - 2023 kama sehemu ya usaidizi wake wa ushauri wa kisheria wa mara kwa mara wa kuhusu ushirikiano wa biashara wa jumuiya hiyo.

Aliongeza kuwa kama hatua ya kwanza, Soko la Pamoja la Bidhaa na Huduma la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC CSG Scan) 2022 - 2023, kampuni hiyo inatathmini hatua za udhibiti kulingana na sheria, notisi za kiutawala, maagizo, zilizochukuliwa na nchi tano Wanachama wa Jumuiya ambazo zinaathiri usafirishaji huru wa mtaji, bidhaa na huduma katika Soko la Pamoja katika kipindi cha Januari mpaka Desemba, 2022.

Alizitaja nchi wanachama zilizozingatiwa katika uzinduzi na uchunguzi wa awali wa Huduma na Bidhaa za EAC wa kila mwaka kuwa ni Kenya, Rwanda, Tanzania, Sudan Kusini na Uganda.

"Mipango iliyopo ni ALP East Africa kutoa ripoti ya namna hii kila robo ya mwaka," alisema.

Ripoti hiyo imezinduliwa kama utangulizi mpana wa ALP East Africa katika nchi kadhaa wanachama wa EAC na kuzitaka kujikita katika huduma na bidhaa za pamoja chini ya soko la pamoja, manufaa yake makubwa kwa hatua za maingiliano ya kibiashara ya Sekretarieti za EAC, Baraza la Sheria la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Baraza la Mawaziri, na taasisi nyingine za kijumuiya.

## Mkakati kurudisha hekta milioni 5.2 za uoto asili waiva

**Na Jenifer Gilla**

WAKALA wa Misitu Tanzania (TFS) unatarajia kuzindua mkakati utakaowezesha kurudisha hekta milioni 5.2 za uoto wa asili ili nchi nzima kufidia hekta 469,000 zilizopotea.

Akizungumza na wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) wiki iliyopita, Mkuu wa Sehemu ya Utangazaji Utalii Ikolojia wa TFS, Anna Lauwo, alisema waliandaa mkakati huo kwa kushirikiana na wadau wengine wa mazingira Tanzania bara na Zanzibar.

Alitaja baadhi wa wadau walioshirikiana nao kuandaa mkakati huo kuwa ni Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), na Ofisi Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Lauwo alisema lengo la kurudisha uoto huo ni kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi zinazikumba dunia na kwamba Tanzania imeshaanza kuona matokeo ikiwamo mafuriko na ukame vinavyosababisha hali ya maisha kuwa ngumu. Pia alitaja sababu nyingine kuwa ni ahadi waliotoa kwa nchi wanachama wa mabadiliko ya hali ya hewa Afrika mwaka 2018 ya kurudisha hekta milioni 100 za utoto asili ili kukabiliana mabadiliko hayo duniani.

Alisema ili kutimiza ahadi hiyo nchi hizo zilitengeneza mkakati walioutia AFR 100 ambapo kila mwanachama alitakiwa atoe ahadi kiwango gani cha uoto asili hizo kitarudisha ili kutimiza lengo la kurudisha hekta 100 kama bara.

Kabla ya kuwapo kwa mkakati huo, alisema walishaanza kutekeleza mikakati iliyokuwapo ikiwamo kutunza misitu iliyopo kwa ajili ya biashara ya kuuza hewa ya ukaa, ambayo ni makubaliano kati ya nchi wanachama ulimwenguni kuwa nchi zilizoendelea zitazilipa pesa nchi zinazoendelea kwa kuwa na miti mingi inayonyonya hewa chafu wanayoizalisha kupitia viwanda.

Alisema misitu inafanya kazi kubwa katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kuwa inazalisha hewa ya oksijen inayofanya kazi ya kusafisha hewa chafu inayozalishwa sababu mbalimbali ikiwamo viwanda vikubwa.

"Kwa hiyo nchi zile ambazo hazijaharibu mazingira sana ikiwamo za Afrika ziliambiwa ziendelee kutunza miti hiyo na zile nchi ambazo zimeshaharibu kwa kiasi kikubwa zitulipe kwa utunzaji huo," alisema. Pia alisema pia wanashirikiana na vijiji vilivyozungukwa na misitu katika utunzaji huo, baadhi ya vijiji wamevipa umiliki wa rasilimali hiyo na kuwasimamia ili kuhakikisha wanaitunza miti hiyo kwa manufaa ya nchi.

Vilevile, alisema wamewapa elimu ya namna wanavyoweza kunufaika na misitu hiyo bila kuiharibu, ikiwamo kufuga nyuki ili wavune asali kwa ajili ya biashara, matunda na dawa zinazopatikana katika rasilimali hiyo.

Kadhalika, alisema walipandisha hadhi ya misitu kutoka misitu ya kawaida hadi kiwango cha juu cha hifadhi ambayo inatumika shughuli za utalii na uhifadhi mazingira hivyo shughuli za kijamii haziruhusiwi zaidi ya hoteli ndogo za miti.

Alisema miti inafanya kazi kubwa katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kuwa inazalisha hewa ya oksijen inayofanya kazi ya kusafisha hewa chafu inayozalishwa sababu mbalimbali ikiwamo viwanda vikubwa.

Akichangia mada, Meneja wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Shirika lisilo la kiserikali la RTI ambao ni Mshirika mtekelezaji wa mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili, John Norohna, alisema takwimu zinaonyesha inakadiriwa asilimia 80 ya Watanzania wanategemea maliasili nchi kiuchumi na kijamii.

Alisema kutokana na hali hiyo kuna haja ya kuwekeza nguvu kubwa kwenye kutunza rasilimali hizo ili zisiendelee kuharibika ikiwamo kuja na teknolojia itakayokuwa mbadala ili kuondoa utegemezi wa rasilimali kwa jamii ikiwamo taa na majiko ya sola.



## Mgogoro ardhi wamwibua RC

**Na Hamida Kamchalla,** KILINDI

MGOGORO wa uuzaji ardhi unaotishia amani ya wakazi wa vijiji Gitu na Ngobole, Kilindi mkoani Tanga, umemwibua Mkuu wa Mkoa huo, Waziri Kindamba, kuingilia kati na kusitisha taratibu zote za uuzaji hadi serikali itakapomaliza kuutatua.

Akiwa katika eneo lenye mgogoro mwishoni mwa wiki, Mkuu huyo wa mkoa aliagiza Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Gitu (VEO), kusimama kuuza maeneo yote yenye mgogoro, mpaka hapo serikali itakapokuja na majibu.

"Uamuzi huu wa kusitisha uuzaji ardhi katika maeneo yote yenye mgogoro, unalenga kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa mgogoro uliopo ili kuzuia uwezekano wa kuibuka mapigano ya wenyewe kwa wenyewe. Naonya hapa kwamba, yeyote atakayeenda kinyume na agizo hili sheria kali zitachukuliwa dhidi yake," alisema Kindamba.

Mgogoro huo wa ardhi baina ya serikali za vijiji na wananchi, umedumu kwa miaka 17 sasa, jambo ambalo serikali imeahidi kuupatia ufumbuzi wa kudumu hadi kufikia mwezi Julai mwaka huu.

Aidha, Kindamba alidokeza kuwa tayari amepokea mapendekezo yaliyotolewa na Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Tanga, na kwamba kwa sasa anakwenda kukaa pamoja na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ngazi ya Mkoa ili kuona namna nzuri ya kuyatekeleza na hatimaye kuja na suluhisho la mgogoro huo.

Akielezea kwa kina kuhusu mgogoro huo, Ofisa Ardhi wa Wilaya ya Kilindi, Natus Manumbu, alisema vijiji hivyo viwili vya Gitu na Ngobole, vinaitenganisha mikoa miwili ya Tanga na Manyara.

Kutokana na kuwapo kwao pembezoni, suala la mwingiliano wa mipaka umezalisha mgogoro mwingine, ambao unahusu wakulima na wafugaji waliopo katika maeneo hayo.

"Kero kubwa inayojitokeza kwa mipaka hii iliyoko kwenye ramani, inaonekana kuna makazi ya Kijiji cha Gitu, ambayo yameenda mpaka eneo la Kiteto na Simanjiro (Manyara), ambayo yapo pia ndani ya Kijiji cha Ngobole.

# Mwanafunzi abuni kifaa kubaini wezi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWANAFUNZI wa kike wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Nauriya Salim Abdallah, amebuni kifaa maalum kinachopiga kelele kwenye simu ya kiganjani ili kumwarifu mfugaji kama kuna mwizi kibandani.

Kutokana na ubunifu huo, ameiomba serikali kuwaunga mkono wanafunzi wabunifu kama yeye ili kusaidia jamii kuondokana na matatizo yanayoikabili katika masuala mbalimbali.

Nauriya mwishoni mwa wiki, aliwavutia mamia ya watu jijini Arusha kwenda kushuhudia ubunifu huo katika kilele cha maonyesho ya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi yaliyoandaliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

Akizungumzia ubunifu wake alisema: "Kifaa hiki kizuri endapo wafugaji watakifunga kwenye mabanda yao na kuunganishiwa mfumo kwenye simu itawaaidia kuondokana na hasara za wizi wa kuku wanaofanyiwa," alisema.

Kutokana na mafanikio hayo, Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Prof. Shadrack Mwakalila, alisema chuo hicho kinatoa mchango mkubwa kwa taifa, ikiwamo utoaji wa maarifa kwa vijana ili waweze kujiajiri na kuondokana na dhana ya kutegemea kuajiriwa.

Kwa mujibu wa Prof. Mwakalila, elimu wanayowapatia vijana wao imezaa matunda kwa vijana wengi kujiajiri, akisisitiza kuwa vijana wengi baada ya kuwapatia elimu chuoni humo, huja na bunifu mbalimbali zenye manufaa kwa jamii na taifa, na zinapoingia sokoni huzalisha ajira.

Mojawapo ya ubunifu huo ni utengenezaji mfumo wa umwagiliaji, usiohitaji mkulima kukaa shambani, ikiwamo mfumo wa kusaidia kufukuza ndege wakiingia shambani na kifaa maalum kinachowekwa katika banda la kuku, kwa ajili ya kudhibiti wizi wa kuku.

"Kutokana na ubunifu mbalimbali kuwa nzuri sisi chuo tutashirikiana na taasisi za fedha ili kuwezesha bunifu zinazozalishwa ziwe na tija na kuzalisha ajira zaidi kwani zina manufaa makubwa kwa jamii," alisema.




Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhamed (kushoto), akipokea zawadi kutoka kwa Ofisa wa Mamlaka ya Elimu TEA, Selanda Jamadari (kulia), alipotembelea banda la TEA katika maonesho ya Elimu ya Ufundi yanayofanyika jijini Arusha viwanja vya Sheikh Amri Abeid. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwekezaji kutoa dola 56,000 ushirika

**Na Godfrey Mushi,** HAI

BODI ya Chama cha Ushirika wa Mazao cha Lukani/Losaa AMCOS, imesema uwekezaji ilioingiwa na mwekezaji mpya wa Shamba la Boloti, kampuni ya Kuza Africa Limited, itakipatia chama hicho Dola za Marekani 56,000, Juni 30 kila mwaka kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya chama na jamii inayozunguka vijiji hivyo viwili.

Mwenyekiti wa chama hicho, Ebenetho Munuo, akizungumza jana katika mahojiano maalum na Nipashe kuhusu uwekezaji huo, alisema mwekezaji huyo kwa sasa anapambana na amejitahidi kuyafufua mashamba ya kahawa yaliyokuwa chini ya Lukani/Losaa AMCOS Ltd.

Alisema kwa sasa chama hicho kinajiandaa kupokea pia mradi wa ufadhili wa USADF kutoka Marekani mwezi Julai mwaka huu, baada ya bodi hiyo kuomba ufadhili wa kugharamia ujenzi wa kiwanda cha kahawa, bustani ya miche pamoja na wakulima kupatiwa pembejeo.


"Haya ni mafanikio makubwa na kimsingi matarajio yetu kwa sasa kutokana na mipango ya muda mrefu tuliyonayo ni kukamilisha ujenzi wa kiwanda chetu cha kahawa na kufufua mfereji wa asili wa Metrum ili kupata maji ya kutosha kumwagilia mazao yetu. Mfereji huo wa Metrum, unavinufaisha hasa vijiji vitano vya Kata ya Masama Magharibi.

"Lakini pia kuendelea kujenga vibanda kama vitega uchumi katika eneo lenye stoo (Lawate) kwa kutumia sehemu ya fedha za pango toka shamba la Boloti," alisema.

Hata hivyo, Munuo alisema mwekezaji huyo aliahidi kulipa Dola za Marekani 6,000 Agosti mwaka jana lakini bado hajatekeleza ahadi hiyo kwa ajili ya maendeleo ya jamii.

Kwa mujibu wa Munuo, ujenzi wa kiwanda cha kahawa (CPU Factory), unaendelea ili kukidhi vigezo vya kuzalisha kahawa maalum kwa kujenga miundombinu ya majengo na maji, mfereji wa maji, kukamilisha visima, ofisi, vitendea kazi na chekecheke.

Kwa msimu wa mwaka 2023/24, chama hicho pia kimepanga kuanza kununua kahawa kwa bei ya awali kwa Sh.3,000 na maganda Sh. 6,000 kwa kilogramu moja na baadaye ilipe nyongeza na mabaki baada ya mauzo kukamilika. Alisisitiza kuwa hali hiyo imetokana na kuyumba kwa bei za masoko ya ndani na nje ya nchi.





## Mkataba wa utekelezaji umeme jua watiwa saini

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

KAMPUNI ya SSI Energy Tanzania na Kampuni ya Ujenzi ya Sinohydro zimetia saini mkataba wa makubaliano ya utekelezaji wa mradi wa umeme jua wa megawati 10 wilayani hapa.

Umeme utakaozalishwa utatumiwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) katika kituo cha Buzwagi kilichoko wilayani Kahama pamoja na kuingizwa katika gridi ya taifa ili kuongeza uzalishaji.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuingia kwa mkataba huo, Meneja Mkazi wa SSI Energy Tanzania Ltd, Dk. Nancy Shadrack, alisema ujenzi wa kituo hicho utakamilika Desemba, mwaka huu. Alisema umeme utakaozalishwa utatumika kwenye makazi, viwandani, ofisini, shuleni na hospitalini pamoja na kuupanua mji wa Kahama kiuchumi.

Dk. Shadrack alisema umeme utakaozalishwa katika kituo hicho pia utasaidia kuongeza uzalishaji katika viwanda vidogo pamoja na kuboresha maisha ya wakazi wa Kahama.

"Tunajisikia furaha kushirikiana na Sinohydro katika ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa jua hapa Kahama, Hatua hii ni kubwa kwa ustawi na maendeleo ya Tanzania," alisema.

Akizungumza baada ya utiaji saini huo, Mwakilishi wa Synohydro Tanzania, Wu Peng, alisema mradi huo utasaidia kuongeza uzalishaji wa umeme katika gridi ya taifa pamoja na upatikanaji wa umeme wa uhakika.

"Synohydro ni mojawapo ya kampuni kubwa za ujenzi duniani hivyo inazingatia na kuchukua tahadhari zote za uhifadhi wa mazingira kwa faida ya kizazi kijacho, Katika mradi huu hakutakuwa na uchafuzi wowote wa kimazingira," alisema Peng.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa SSI, Nick Richardson, alisema: "Wakati Tanzania inapiga hatua katika uhifadhi wa mazingira tunatambua madhara ya gesi ya kaboni na ndiyo sababu Kampuni ya Sinohydro inajiandaa kuzalisha umeme rafiki utakaotumika katika viwanda na makazi ya watu."

Alisema katika kufanikisha hilo ndiyo sababu wameshirikiana na Kampuni ya Synohydro ambayo ina ujuzi wa kutekeleza miradi kwa wakati.

Kampuni ya SSI Energy Tanzania ilianzishwa mwaka 2017, kwamba ujenzi wa mradi wa umeme jua wa Kahama ni kwanza kuutekeleza na unatarajia kukamilika Desemba 2023.

Kampuni ya Sinohydro inamilikiwa na serikali ya China kwamba ipo Tanzania kwa zaidi ya miaka 26.

# DC acharuka kukithiri matukio mauaji

**Na Samson Chacha,**
TARIME

MKUU wa Wilaya ya Tarime, Kanali Michael Mtenjele, ameonyesha kukerwa na vitendo vya uhalifu yakiwamo mauaji ya kutumia silaha za moto ambayo yamekuwa yakiripotiwa wilayani hapo.

Kutokana na kukithiri kwa matukio hayo, amewataka viongozi na watendaji kuhimiza kuanzishwa vikundi vya ulinzi shirikishi kwa lengo la kusaidiana na polisi kudhibiti vitendo hivyo.

Kanali Mtenjele alisema hayo juzi katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji wa Tarime na kusema madiwani na watendaji kata wanatakiwa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha vitendo hivyo vinadhibitiwa na wahalifu wanakamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Nawaagiza nendeni katika maeneo yenu kwa kushirikiriana na wenyeviti wa vijiji anzisheni vikundi vya ulinzi shirikishi.

Mtapata ushirikiano kutoka polisi kata walioko katika maeneo yenu na tutapita na kamati yangu ya ulinzi na usalama kila kata kuhakiki kama vikundi hivyo vimeundwa na vinafanya kazi," alisema Kanali Mtenjele.

Kanali Mtenjele pia alihimiza viongozi wa ngazi za kata na vijiji kuhamasisha wananchi hususani wazazi kuchangia chakula kwa wanafunzi shuleni hali itakayoongeza ufaulu kwa wanafunzi sambamba na kufuatilia mienendo ya watoto wao kujiepusha na vitendo visivyo na maadili kwa jamii.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Daniel Komote, aliahidi kutekeleza maagizo hayo huku akieleza kupokea hoja za madiwani ikiwamo kuwaondoa watu waliojenga jirani na mito na ndani ya hifadhi ya barabara na kuendesha shughuli za kibinadamu hali inayoharibu mazingira na kusababisha mafuriko ya mara kwa mara yanayoleta madhara ikiwamo vifo.

Pia alizitaka idara za ardhi na mazingira kufuatilia watu waliojenga karibu na mito bila kufuata taratibu kati ya mita 30 na 60 hali itakayosaidia kupunguza madhara yatokanayo na mvua zinazojaza vyanzo hivyo vya maji.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Gwabina Ntovya, alisema katika kipindi cha Mei wamepokea Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 42 vya madarasa, matundu 54 ya vyoo , madarasa ya awali na kuanzisha ujenzi wa shule mpya mbili, vichoma taka na jengo la utawala katika shule huku akihimiza ufuatiliaji katika utekelezaji wa miradi hiyo.




Wauguzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama na wanachuo wa Chuo cha Uuguzi Kahama mkoani Shinyanga, wakiwa katika maandamano ya amani ya kusherehekea Siku ya Wauguzi kiwilaya huku wakibeba mabango yenye ujumbe mbalimbali juzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Tani sita bidhaa hatarishi zateketezwa

**Na Neema Emmanuel,**
NYAMAGANA

TAKRIBANI tani sita ya bidhaa mbalimbali vikiwamo vipodozi vyenye viambata sumu zenye thamani ya Sh. milioni 100 zimeteketezwa baada ya kuondolewa sokoni kutokana na kutokidhi matakwa ya viwango.

Bidhaa hizo ziliteketezwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika dampo la Buhongwa juzi, jijini Mwanza, baada ya kukamatwa kwenye mikoa sita ya Kanda ya Ziwa.

Akizungumza wakati wa utekelezaji wa bidhaa hizo, Meneja wa TBS Kanda ya Ziwa, Happy Brown, alitaja bidhaa zilizoteketezwa mbali na vipodozi vyenye viambata vya sumu ni pamoja vyakula vilivyokwisha muda wa matumizi.

Kuhusu vipodozi vilivyoteketezwa, Brown alisema vilipigwa marufuku kutumika nchini kutokana na kuwa na madhara ya kiafya kwa watumiaji ikiwamo kusababisha kansa.

Alisema bidhaa hizo zilikamatwa wakati wa ukaguzi uliofanywa na maofisa wa TBS kwenye masoko, maduka na kwenye maghala katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera, Geita, Mara na Simiyu na halmashauri zake katika kipindi cha Oktoba, mwaka jana na Machi, mwaka huu.

Akieleza hatua za kisheria zilizochukuliwa kwa waliokamatwa na bidhaa hizo, Ofisa Usalama wa Chakula wa TBS Kanda ya Ziwa, Tunu Mwansulama, alisema ni pamoja na kulipa faini ambayo inatumika katika kuteketeza bidhaa hizo kwa gharama hizo hazilipwi na serikali.

Nipashe
Spotika




KLABU TANO ZILIZOSHINDA UEFA MARA NYINGI ZAIDI UK. 12-13



# WAKALI 10 WA UWIANO WA MABAO ULAYA

NEYMAR

**LIVERPOOL,** England

SASA tunakwenda kushuhudia Fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kati ya Manchester City dhidi ya Inter Milan.

Na linapokuja suala la uwiano wa mabao kwa kila mchezo kati ya wachezaji walio na mabao 30 au zaidi, makala haya inawachambua wachezaji 10 bora zaidi.

**10. Neymar (mabao 43) – Uwiano wa 0.53 kwa mchezo**

Mwanasoka ghali zaidi katika historia ya mchezo huo aling'ara zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Barcelona na Paris Saint-Germain.

Neymar aliifanya timu hiyo ya Hispania kutwaa ubingwa wa Ulaya msimu wa 2014-15, akifunga mabao 10 katika mechi 12, na saba kati ya hizo akifunga kuanzia kwenye robo fainali na kuendelea.

**9. Mohamed Salah (mabao 44) – Uwiano wa 0.56 kwa mchezo**

Mohamed Salah alijitambulisha kwenye Ligi ya Mabingwa kule Basel, akifunga nyumbani na ugenini dhidi ya waajiri wake wa wakati huo Chelsea katika hatua ya makundi ya msimu wa 2013-14.

Mmisri huyo sasa amempita Steven Gerrard kama mfungaji bora wa muda wote wa Liverpool katika michuano hiyo ya Ulaya akiwa amefunga mabao 42.

**8. Filippo Inzaghi (mabao 46) – Uwiyano wa 0.57 kwa mchezo**

Filippo Inzaghi ni mshindi mara mbili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na alikuwa mfungaji wa pili katika msimu wa 2002-03 akiwa na mabao 10.

Muitaliano huyo pia alichaguliwa kuwa Mchezaji Bora wa Mechi katika fainali ya mwaka 2007 baada ya kufunga mabao mawili katika ushindi wa 2-1 wa AC Milan dhidi ya Liverpool.

**7. Karim Benzema (mabao 90) – Uwiano wa 0.59 kwa mchezo**

Benzema ndiye mfungaji bora wa nne katika historia ya Ligi ya Mabingwa na alifunga mara 15 katika kampeni ya ushindi ya Real Madrid msimu wa 2021-22.

Mshindi huyo wa Ballon d'Or alianza kwa mara ya kwanza katika mashindano hayo akiwa na umri wa miaka 17 kule Lyon dhidi ya Rosenborg ambako alifunga bao lake la kwanza.

**6. Kylian Mbappe (mabao 40) – Uwiano wa 0.66 kwa mchezo**

Kylian Mbappe alijitambulisha kwa mara ya kwanza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Monaco, akifunga mabao sita katika mechi tisa wakati ilipotinga nusu fainali msimu wa 2016-17.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 ameendelea kutamba pale PSG, huku hat-trick yake dhidi ya Barcelona msimu wa 2020-21 ikiwa ni kiwango chake cha kukumbukwa zaidi hadi sasa.

**5. Ruud van Nistelrooy (mabao 56) – Uwiano wa 0.77 kwa mchezo**

Ruud van Nistelrooy hakuwahi kunyanyua taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini alishinda Kiatu cha Dhahabu akiwa na Manchester United msimu wa 2002-03 kwa kufunga mabao 12.

Mholanzi huyo pia anashikilia rekodi ya kuwa mchezaji aliyefunga mabao 40 kwa haraka zaidi, akifanikiwa kufunga katika mechi 45 pekee.

**4. Cristiano Ronaldo (mabao 140) – Uwiano wa 0.77 kwa mchezo**

Mafanikio ya Cristiano Ronaldo katika Ligi ya Mabingwa Ulaya hayana kifani. Yeye ni mshindi mara tano, mfungaji bora wa rekodi akiongoza kwa asisti (40).

Mchezaji huyo alifunga mabao 17 msimu wa 2013-14 - wakati Real Madrid iliposhinda - bado ni idadi kubwa zaidi kuwahi kufungwa na mchezaji katika msimu mmoja.

**3. Lionel Messi (mabao 129) – Uwiano wa 0.79 kwa mchezo**

Lionel Messi amekuwa mchezaji wa kudumu katika Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu alipoanza mwaka 2005 na anashika nafasi ya tatu kwenye orodha ya wachezaji waliocheza mechi nyingi zaidi (mechi 163) nyuma ya Ronaldo na Iker Casillas.

Msimu uliofanikiwa zaidi kwa mshindi huyo wa Kombe la Dunia ulikuwa ule wa 2011-12 akiwa Barcelona, ambapo alifunga mabao 14 katika mechi 11 alizocheza.

**2. Robert Lewandowski (mabao 91) – Uwiano wa 0.82 kwa mchezo**

Robert Lewandowski aliiongoza Bayern Muni kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa msimu wa 2020-21 kwa kufunga mabao 15, idadi yake kubwa zaidi katika msimu mmoja.

Raia huyo wa Poland kabla ya hapo aligonga vichwa vya habari kwenye michuano hiyo akiwa Borussia Dortmund, pia, akiandikisha ushindi wa mabao manne katika nusu fainali ya 2012-13 dhidi ya Real Madrid.


**1. Erling Haaland (mabao 35) – Uwiano wa 1.20 kwa mchezo**

Ikiwa Haaland atadumisha kiwango chake cha kushambulia na kuepuka majeraha mabaya, atavuka rekodi ya Ronaldo ya mabao 140.

Raia huyo wa Norway ni mmoja wa wachezaji watatu pekee waliofunga mara tano kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa - wengine wawili wakiwa Messi na Luiz Adriano.

## ISIKUPITE

BEKI wa Manchester City, Kyle Walker amesema Arsenal waliwapa wakati mgumu kwenye mbio za ubingwa na wanastahili pongezi lakini makosa madogo waliyoyafanya yamewapa wao (Manchester City) nafasi ya kutetea ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo. Amesema aina ya ubora wa wachezaji walionao umetoa nafasi ya kumaliza ligi wakiwa juu na kutangaza ubingwa msimu huu huku wakiwa na mchezo mko-






# KLABU TANO ZILIZOSHINDA UEFA MARA NYINGI ZAIDI

**LONDON,** England

LIGI ya Mabingwa Ulaya ni njia 'takatifu' kwa wachezaji na makocha mashuhuri barani Ulaya.

Mashindano hayo yanayojulikana kama Kombe la Uefa yanayotumia mtindo wa mtoano yanaunda kumbukumbu zisizosahaulika na kwa wale waliobahatika kubeba kombe.

**Lakini ni klabu gani zimefurahia mafanikio zaidi kwenye michuano hiyo mikubwa zaidi kwa ngazi ya Klabu barani Ulaya?**

Makala haya yanakuchambulia klabu tano zilizotwaa mara nyingi zaidi taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**Real Madrid - 14**
**Kwa mara ya kwanza: 1956**
**Kwa mara ya mwisho: 2022**

Ukweli wa kufurahisha: Real Madrid ndio inayoshikilia rekodi ya kushinda taji hilo mara nyingi mfululizo kwa mara tano (mwaka 1956 hadi 1960).

Los Blancos hao bila shaka wanatakiwa kupewa heshima ya kuwa timu iliyofanikiwa zaidi katika historia ya shindano hilo.

Klabu hiyo ya Hispania imetoa nyakati za kufurahisha zaidi kwenye mashindano hayo ya Ulaya, haswa bao la ushindi la Zinedine Zidane, ambalo liliipata taji la tisa klabu hiyo mwaka 2002.

Gareth Bale pia alifunga bao la kukumbukwa la tiktaka katika ushindi wao wa mwaka 2018, akiachia mkwaju wa juu kwa juu uliompita golikipa wa Liverpool, Loris Karius.

**AC Milan - 7**
**Kwa mara ya kwanza: 1963**
**Kwa mara ya mwisho: 2007**

Ukweli wa kufurahisha: AC Milan ilikuwa timu ya kwanza ya Italia kushinda Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 1963.

Labda ushindi wa kukumbukwa zaidi wa Milan kwenye Ligi ya Mabingwa ulikuja mwaka wa 2007, waliposhinda kizingiti cha kiakili cha kuishinda Liverpool katika marudio ya fainali ya mwaka 2005.

Filippo Inzaghi alifunga mabao mawili mjini Athens na kukamilisha ushindi wa 2-1 huku wachezaji kama Kaka, Clarence Seedorf na Paolo Maldini wakiwa nyota kwenye mchezo huo.

Mapema katika muongo huo, Andriy Shevchenko alicheza vyema katika fainali ya mwaka 2003 ambapo ilizikutanisha klabu pekee za Italia, Milan dhidi ya Juventus. Raia huyo wa Ukraine alifunga mkwaju wa penalti ya ushindi pale kwenye dimba la Old Trafford nchini England na kuipa Milan taji la sita.

**Bayern Munich - 6**
**Kwa mara ya kwanza: 1974**
**Kwa mara ya mwisho: 2020**

Ukweli wa kufurahisha: Ushindi wa Bayern Munich wa 1974 ulikuwa wa kwanza na kwa mara ya kwanza na kipekee fainali kuamuliwa kwa mechi ya marudiano.

Baada ya sare ya 1-1 mjini Brussels dhidi ya Atletico Madrid, Franz Beckenbauer alinyanyua kombe siku mbili baadaye kutokana na ushindi wa 4-0.

Hakuna kitu kitamu kama kuwashinda wapinzani wako kwenye hatua kubwa zaidi na Bayern Munich walifanya hivyo walipoishinda Borussia Dortmund mnamo mwaka 2013, kwa hisani ya bao la dakika ya mwisho kutoka kwa Arjen Robben.

Mnamo 2001, Bayern ilishinda Valencia katika mchezo uliojaa mikwaju ya penalti. Mechi hiyo ilimalizika kwa sare ya 1-1 huku timu zote zikifunga goli lakini ni Bayern walioibuka kidedea kwa mikwaju ya penalti na kufanikiwa kutwaa taji lao la nne.

Mapema mwaka 2020 ilishuhudia Bayern wakitwaa taji lao la sita, wakiishinda Paris Saint-Germain katika fainali pekee iliyochezwa bila mashabiki kutokana na janga la mlipuko wa virusi vya Corona.

**Liverpool - 6**
**Kwa mara ya kwanza: 1977**
**Kwa mara ya mwisho: 2019**

Ukweli wa kufurahisha: Liverpool ndio klabu iliyofanikiwa zaidi kutoka nchini England kwenye michuano hiyo, ikishinda fainali sita kati ya 10 iliyoweza kufuzu.

Fainali ya Liverpool dhidi ya AC Milan mwaka 2005 bila shaka ilikuwa hitimisho kubwa zaidi katika historia ya mashindano hayo.

Hatimaye wakishinda kwa mikwaju ya penalti, Liverpool walitoka nyuma ya mabao 3-0 kipindi cha mapumziko. Lakini kipindi cha pili waliweza kusawazisha mabao hayo na fainali kuamuliwa kwa changamoto ya mikwaju ya penalti na Liverpool wakashinda kwa kile kinachoitwa 'miujiza ya Istanbul'.

Mwaka 2019, Mohamed Salah na Divock Origi walikuwa wameamua mbele ya lango walipoishinda Tottenham kule jijini Madrid nchini Hispania, lakini walipoteza kwa 1-0 kwa Los Blancos katika mchezo mwingine wa fainali msimu uliopita.

**Barceloba - 5**
**Kwa mara ya kwanza: 1992**
**Kwa mara ya mwisho: 2015**

Ukweli wa kufurahisha: Ushindi wa kwanza wa Barcelona mwaka 1992 ulikuwa toleo la mwisho la Kombe la Ulaya kabla ya mashindano hayo kubadilishwa kuwa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lionel Messi ameng'ara mara nyingi katika matukio kadhaa ya ajabu na ya kuvutia kwenye mafanikio ya Barcelona katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mwaka 2008, mpira wake wa kichwa ulipatia Barcelona ushindi wa kwanza baada ya miaka 16 wakati kikosi cha Pep Guardiola kilipowashinda mabingwa watetezi Manchester United mjini Rome chini Italia.

Miaka mitatu baadaye, Mashetani Wekundu walikuwa tena upande usiofaa dhidi ya Blaugrana, huku Messi akiibuka na ushindi wa mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Wembley.

Mnamo mwaka wa 2015, nyota huyo wa Argentina dhidi ya Jerome Boateng na Manuel Neuer aliiweka timu hiyo ya Catalunya kwenye fainali nyingine, ambapo walikwenda kuifunga Juventus mjini Berlin nchini Ujerumani.

## Nukuu

"Ni siku ya huzuni sana na hisia nyingi ngumu. Tulipoteza mchezo na tukapoteza ubingwa baada ya miezi 10 na nusu kuupigania na miezi tisa na nusu kuukaribia, tulijenga hamasa na imani kubwa kuwa tunaweza kufika mbali na kushinda, mwisho tukashindwa, kwanza niwapongeze Man City, ni mabingwa na wanastahili kuwa mabingwa," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta akizungumzia namna walivyoshindwa kutwaa ubingwa msimu huu licha ya kuongoza ligi kwa muda mrefu.**



"Kila mmoja anafahamu vizuri hali yangu hapa, nina mkataba mpaka mwishoni mwa msimu wa 2014 na nataka kuendelea kubaki hapa..., Ndio nimehakikishiwa kuendelea kuwepo hapa". **Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti akizungumzia mustakabali wake kwenye timu hiyo baada ya kutolewa katika hatua ya nusu fainali dhidi ya Manchester City.**



"Sijali na siangalii nini kitawatokea Liverpool, tunajiangalia sisi kwa sasa, lazima tufanye kazi yetu vizuri na kupata matokeo chanya kwenye mechi zilizobakia na kuona mwisho wa msimu tupo kwenye nafasi gani". **Kocha wa Manchester United, Ten Hag akizungumzia mchuano wa kuwania kumaliza katika Top 4 kati yao na Liverpool.**






# MAMBO MA5 USIYOYAJUA KUHUSU USM ALGER

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania Bara, Yanga, wanakwenda kukutana na timu ya USM Alger ya Algeria kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Shirikisho itakayopigwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Jumapili ijayo na marudiano yatakuwa nchini Algeria kwenye Uwanja wa Juillet wa Tano, Juni 3.

Watanzania wengi hawaifahamu vizuri timu hii, japo imeshawahi kucheza mechi mbalimbali za kimataifa. Je, wawakilishi wa Tanzania Yanga wanakutana na timu ya gani? Mwandishi wa makala haya anakuletea historia, rekodi na takwimu kadhaa kuhusu klabu hiyo.

### Imetwaa ubingwa wa ligi mara nane

Jina kamili la klabu hiyo ni Union Sportive de la Medina d'Alger, kwa kifupi ndiyo inatamkwa USM Alger, klabu hii imeanzishwa mwaka 1937, miaka miwili tu baada ya kuanzishwa kwa Yanga. Ipo kwenye Ligi Kuu ya Algeria na Uwanja wake wa nyumbani ni Omari Hamadi wenye uwezo wa kuingiza watazamani 17,500.

Imeshatwaa ubingwa wa Ligi Kuu nchini mwao mara nane mpaka sasa ikiwa ni misimu ya 1962/63, 1995/96, 2001/02, 2002/03, 2004/05, 2013/14, 2015/16, na 2018/19.

Imeshika nafasi ya pili kwyenye Ligi Kuu mara nne, mwaka 1997/98, 2000/01, 2003/04, na 2005/06.

**JE, WAJUA?**

WAPINZANI wa Yanga katika fainali ya kombe la Shirikisho Afrika, USM Alger ya Algeria walicheza hatua ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 2015 dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. USM Alger ilichapwa jumla ya mabao 4-1 na kushuhudia ubingwa ukichukuliwa na TP Mazembe iliyokuwa na Mshambuliaji Mtanzania Mbwana Samatta.

### Ilifika fainali Ligi ya Mabingwa 2015

Mwaka 2015 ilifanikiwa kutinga hatua ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini kwa bahati mbaya ikafungwa jumla ya mabao 4-1 na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Ilichapwa mabao 2-1 nyumbani na ilipokwenda Lubumbashi iliambulia kipigo kingine cha mabao 2-0 na kulikosa kombe hilo. Na hayo ndiyo mafanikio makubwa zaidi ya klabu hiyo.

### Iliteswa na Samatta

Kwenye mechi hizo mbili za fainali USM Alger hawatoweza kumsahau straika wa Kitanzania ambae ni nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta ambaye aliwafunga mabao mawili, kila mechi akishindilia bao moja.

Fainali ya kwanza ilichezwa Oktoba 31, 2015 kwenye Uwanja wa Omari Hamadi nchini Algeria, ilihushuhudiwa na watazamani 15,000, USM Alger ikilala mabao 2-1, yaliyofungwa na Ranford Kalaba dakika ya 28 na Samatta kwa mkwaju wa penalti dakika ya 79, huku bao lao la kufutia machozi likiwekwa ndani ya nyavu na Mohamed Seguer dakika moja kabla ya mechi kumalizika.

Fainali ya mkondo wa pili ilichezwa kwenye Uwanja wa TP Mazembe, Lubumbashi DRC, Novemba 8, 2015 ikishuhudia USM Alger akitandikwa mabao 2-0, Samatta akifunga tena bao kwa mkwaju wa penalti dakika ya 74 na Roger Assale dakika tatu za nyongeza kabla pambano kumalizika, hivyo kufungwa jumla ya mabao 4-1.

### Imeshakutana na Yanga Shirikisho

Fainali hiyo inakwenda kuzikutanisha timu ambazo zimeshawahi kukutana mwaka 2018 kwenye kombe hilo hilo la Shirikisho barani Afrika, zikiwa Kundi D.

Mara ya kwanza ilikuwa Mei 6, 2018, USM Alger ikiikaribisha Yanga, kwenye mechi hiyo, wenyeji walishinda mabao 4-0, yaliyofungwa na Oussama Darfalou, Farouk Chafai, Abderrahmane Meziane na Mohamed Zemmamouche.

Zilikutana tena kwenye mzunguko wa pili Agosti 19, Yanga ikishinda mabao 2-1, mabao ya washindi yakifungwa na Deus Kaseke dakika ya 44 na Heritier Makambo dakika ya 47.

### Nafasi ya nane Ligi Kuu

USM Alger inakamata nafasi ya nane kwenye Ligi Kuu nchini Algeria, ikiwa imecheza mechi 20, ikishinda tisa, sare tano na kupoteza jumla ya mechi sita. Imejikusanyia pointi 32 kwenye ligi hiyo yenye timu 16, inayoongozwa na kinara CR Belouizdad yenye pointi 50.





# Wataka kasi kupambana wizi maudhui

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetakiwa kuweka mikakati ya kupambana na vitendo vya wizi wa maudhui na uharamia kwenye mitandao ya kijamii ili kulinda kazi za wasanii na kampuni mbalimbali ambazo zimekuwa zikiwekeza kiasi kikubwa cha fedha.

Ombi hilo lilitolewa juzi jijini hapa na wadau wa masuala ya usambazaji wa maudhui kwenye runinga pamoja na mitandao ya kijamii wakati wa semina ya siku moja kwa wajumbe wa kamati za kudumu za Bunge iliyoandaliwa na Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA).

Wajumbe hao ni kutoka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo na Kamati ya Sheria Ndogo ambazo ndizo zenye dhamana ya kuisimamia COSOTA.

Johnson Mshana, Mkuu wa Uhusianao DSTV Tanzania, alisema vitendo vya wizi wa maudhui na uharamia kwenye mitandao ya kijamii vimeshika kasi hali ambayo inachangia wamiliki wa maudhui hayo kukosa mapato.

"Wizi huu wa maudhui unasababisha pia serikali yetu kukosa mapato lakini pia wamiliki wa kazi kupoteza fedha nyingi ambazo wangezipata kama hawa wezi wangefuata taratibu za kisheria," alisema.

Pia alisema kutokana na hali hiyo, wanaliomba Bunge kuishauri serikali kuweka mikakati ambayo itasaidia kukomesha vitendo hivyo ili serikali pamoja na wamiliki wa kazi mbalimbali wapate mapato wanayostahili.

Mkuu wa Kitengo cha Sheria na Udhibiti DSTV Tanzania, Atrid Mapunda, alisema wizi wa maudhui limekuwa jambo la kawaida katika maeneo mengi nchini.

"Hivi sasa wizi wa maudhui imeshika kasi sana kwenye hoteli, majumbani hata katika vituo vya polisi watu wanatumia njia zisizo halali kutazama vitu kama muziki, tamthilia bila kulipia lakini pia watu wa 'cable' wamekuwa kikwazo kwetu kwa kusambaza maudhui ambayo hawana hakimilki nayo kinyume cha sheria," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Prof. Kitila Mkumbo, alisema mafunzo hayo yatakuwa nyenzo muhimu kwao katika kuishauri serikali kufanya maboresho kwenye sheria ya hakimiliki.

"Tunashukuru kwa mafunzo haya tumepata mambo makubwa sana na kama inawezekana wabunge wote wangepata mafunzo haya kwakuwa wengi hatujui kama haya mambo tunayofanya kila siku ni wizi na nikinyume na sheria na adhabu zake ni pamoja na faini ya hadi milioni 20," alisema.

Pia alisema kuna haja kwa serikali kuona ni jinsi gani inaweka jitihada za kutosha ili kukomesha vitendo hivyo na kulinda hakimiliki za watu wanaowekeza kiasi kikubwa cha fedha kuandaa maudhui yao.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Ofisi ya Hakimili Tanzania (COSOTA), Doreen Sinare, alisema moja ya jitihada wanazofanya ni kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ili kupunguza vitendo vya wizi wa maudhui nchini na mafunzo hayo kwa wabunge yatakuwa endelevu.



Mkurugenzi Mtendaji wa Airtel Tanzania, Dinesh Balsingh, akifuatilia kwa makini hotuba ya bajeti ya Waziri wa Habari, Mawasiliano 2023/2024 bungeni mjini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watoto 1,800 wakabidhiwa kadi bima afya

**Na Renatha Msungu,** KONGWA

WATOTO 1,800 kutoka vijiji sita wilayani Kongwa mkoani Dodoma, wamekabidhiwa kadi za bima ya afya na wengine 446 wakikabidhiwa vyeti vya kuzaliwa na Shirika la World Vision Tanzania kupitia mradi wa bima ya afya na vyeti vya kuzaliwa (KONGWA AP) unaotekelezwa wilayani hapa.

Vijiji hivyo ambavyo mradi huo unatekelezwa ni pamoja na Mnuku, Mvurungurumo, Mkoka, Mlanje, Makawa na Muungano.

Pia shirika hilo limetoa madawati 90 yenye uwezo wa kukaliwa na wanafunzi 270, katika Shule ya Msingi Mkoka lengo likiwa kuhakikisha watoto wanasoma katika mazingira mazuri.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi kadi hizo vyeti pamoja na madawati, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Mwema, alisema kadi hizo za bima ya afya zitawasaidia watoto kupata matibabu kirahisi katika hospitali mbalimbali ambazo wataenda kutibiwa.

Alisema kadi hizo zitawasaidia wazazi kupunguza gharama ya kutumia fedha wanapokwenda katika vituo vya afya kupata huduma za kitabibu kutoka kwa wataalamu wa afya.

"Tunawashukuru World Vision Tanzania kwa msaada walioutoa kwa watoto kadi za bima ya afya ni muhimu kuwa nazo kwa sababu unatibiwa popote hata kama huna fedha,"alisema Mwema.

Pia aliitaka jamii hususani wazazi kutunza kadihizo ikiwamo kufuata maelekezo ya matumizi watakayopewa na wataalamu wa afya katika vituo mbalimbali vya afya.

Mkuu huyo wa wilaya alisisitiza wazazi kuhakikisha wanafuatilia vyeti vya kuzaliwa vya watoto kwa sababu ni vya muhimu na vinahitajika kila mahali pale wanapofikia umri wa kutafuta fursa mbalimbali.

Mratibu wa Mradi huo, Magrerh Mpwaji, alisema mradi wa maendeleo ya katika eneo la Kongwa unaotekelezwa katika Kata tatu za wilaya ya Kongwa ulianza mwaka 2010 na unategemea kumalizika 2025.

Mpwaji alisema lengo la mradi huo,ni pamoja na kuboresha maisha ya mtoto familia na jamii ya watu wa kata hizo ili watoto wapate afya bora, elimu bora na lishe bora.

Alifafanua zaidi ya kuwa, mradi huo unafanya kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hususani serikali, huku akiishukuru kutokana na kutoa ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa mradi huo.

## Kata zitakazoongoza kwa uchafu kupewa hati chafu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma inatarajia kuanza kutoa hati chafu kwa kata zitakazokuwa vinara wa uchafu kwenye maeneo yao na kushindwa kutunza mazingira na kufanya usafi.

Ofisa Mazingira wa jiji hilo, Dickson Kimaro, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na madiwani kwenye kikao cha baraza baada ya kukabidhi vyeti vya pongezi kwa kata nne zilizofanya vizuri kwa kuweka mazingira safi kati ya 41 zilizopo.

Kimaro alisema kuwa Jiji limedhamiria kutoa hati chafu kwa kata zitakazokuwa chafu ili kuwahamasisha wananchi wao kufanya usafi wa mazingira wa kila siku kwenye maeneo yao.

Alisema, ili kuleta ushindani huo wa kutunza mazingira na kufanya usafi, jiji limetoa vyeti hivyo vya pongezi kwa kata hizo kinara wa safi.

"Jiji la Dodoma kuna kata 41, lakini zilizoonyesha na kutekeleza usafi wa mazingira ni nne tu kati ya hizo na kwenye kikao hiki cha Baraza la Madiwani zitakazostahili kupewa vyeti vya pongezi ni kata ya Ipagala, Chamwino Tambukareli na Mnadani ambazo mitaa yao imefuzu kwa usafi," alisema.

Kimaro aliwaomba wenyeviti wa serikali za mitaa kwa zile kata ambazo hazijapewa vyeti vya pongezi kuendelea kutoa elimu ya umuhimu wa usafi wa mazingira na kuhamasisha wananchi wao ili kujitokeza kwenye usafi.

Naye Juma Mazengo, Diwani wa Kata ya Tambukareli, aliwaasa madiwani ambao kata zao hazikufanikiwa kutoa elimu itakayowahamasisha badala ya vitisho na faini zisizokuwa na mishiko.

Mazengo alisema kupatikana kwa cheti hicho cha pongezi ni kutokana na elimu ya uhamasishaji ambayo iliwafanya wananchi kujitokeza wao wenyewe na kupenda kufanya usafi wa mazingira bila kushurutishwa.

"Niwaombe viongozi wenzangu wa ngazi za kata tuendelee kushirikiana na wananchi wetu katika suala hili la usafi wa mazingira ili jiji letu liwe kinara wa kuwa wasafi kwenye maeneo yote huku ikiwa na ustawishaji wake wa upandaji miti," alisema.





# Waonya kuporomoka soko la pareto

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WADAU wa pareto nchini, wametahadharisha kuwa Tanzania inaweza kupoteza nafasi ya kuwa mzalishaji wa kwanza wa zao hilo barani Afrika na wa pili duniani ikiwa wakulima wataendelea kuuza kwa kampuni likiwa na unyevu wa zaidi ya asilimia 13.

Walitoa angalizo hilo mwishoni mwa wiki kwenye mkutano wa wadau wa pareto uliofanyika jijini Mbeya. Mkutano huo ulikuwa na lengo la kutoa mafunzo kwa zaidi ya mawakala 200 namna ya kuwapa mbinu za kununua na kuuza maua ya pareto yenye ubora ili kuboresha mnyororo wa thamani kuanzia kwa mkulima hadi sokoni.

Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Mbeya, Gideoni Mapunda, alisema kitengo cha mawakala kununua maua ya pareto na kisha kwenda kuziuzia kampuni wakati yakiwa hayajakauka vizuri, kinatishia uhimilivu wa soko la pareto ndani na nje ya nchi.

Mapunda alisema Tanzania ni nchi ya kwanza barani Afrika na ya pili duniani kwa uzalishaji wa pareto lakini katika msimu uliopita zao hilo halikuwa bora kwa kuwa kampuni ziliingia hasara kutokana na kununua maua ambayo hayana kiwango kinachokubalika. "Tumepokea malalamiko kutoka kampuni saba kwamba sumu imepunguza kwenye pareto kwa sababu mawakala wananunua maua ya pareto kwa wakulima ambayo hayajakauka. Sasa hali hii sio nzuri na hizi kampuni zilikuja kuwekeza huku na zinaweza kuondoka,"alisema Mapunda.

Alionya kuwa serikali haitawafumbia macho mawakala ambao watauza maua yaliyo na unyevu wa zaidi ya asilimia 13, huku akibainisha kuwa sheria za nchi ziko wazi na kwamba watakaobainika wanaweza kupata adhabu ya faini au kifungo.

Kaimu Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Ileje, Yona Mbugi, alisema miongoni mwa mambo waliyokubaliana ili kuondoa tatizo hilo ni kukaa meza moja na mawakala pamoja na kampuni zote zinazonunua pareto.

"Kwa sababu kampuni ni nyingi na kuna ushindani, baadhi hununua maua ambayo hayana kiwango hili jambo sio zuri linaharibu taswira ya nchi hata kwa makampuni mengine," alisema.

Mdhibiti wa Pareto kutoka Bodi ya Pareto Tanzania, Edwin Margwe, alisisitiza kuwa bodi inasimamia zao hilo ili kusiwe na upande wowote unaolelewa kutokana na uzembe wa upande fulani.

Alionya kuwa serikali haitasita kuzifutia leseni kampuni ambazo hayatazingatia sheria ya pareto ikiwamo kununua maua yenye unyevu wa zaidi ya asilimia 13.

"Mkakati mkubwa ni kusimamia vituo vyote kuanzia shambani, kwa mawakala hadi kampuni zinazonunua ili kuhakikisha kwenye mikono yote hiyo maua yanapita yakiwa na viwango vinavyokubalika," alisema.

Mwakilishi wa Kampuni ya Pareto Tanzania (PCT), Jerald Joseph, alisema asilimia 30 ya maua waliyoyapata katika msimu wa mavuno uliopita yalikuwa na unyevu wa juu ya asilimia 13.

Alisema hali hiyo ilisababisha PCT kupata hasara ya zaidi ya Sh. bilioni moja kutokana na kuanza kukausha tena maua, hivyo uzito kwenye kilo.

## Wahofia kupoteza mitaji ya biashara

**Na Grace Mwakalinga,** TUNDUMA

WAFANYABIASHARA katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma mkoani Songwe, wamesema wako hatarini kupoteza mitaji baada ya biashara ya mahindi kuzuiwa nchini Zambia kwa madai kuwa nchi hiyo ina akiba ya kutosha kwa sasa.

Serikali ya Zambia ilinunua shehena ya mahindi mwaka 2022 baada ya nchi hiyo kuwa na uhitaji mkubwa wa bidhaa hiyo, hali iliyoilazimu kununua kwa wingi ili kukidhi mahitaji ya wananchi wa Zambia.

Aliyekuwa Mbunge wa Tunduma, Frank Mwakajoka, alisema juzi kwenye mkutano wa hadhara kuwa wafanyabiashara wa Tunduma hawana soko la uhakika la kuuza mahindi yao baada ya Zambia kuwa na mahindi ya kutosha.

Kutokana na hali hiyo, aliiomba serikali kuingilia kati pamoja na kuwatafutia soko la uhakika wafanyabiashara ili mipaka ya kibiashara iendelee kufunguliwa.

"Wafanyabiashara wa Tanzania walianza kununua mahindi Juni 2022 nchini Zambia na kuyauza katika eneo maarufu la biashara la Nakonde lakini cha ajabu ilipofika Novemba 2022, serikali ya Zambia ilianza kugoma kuwapatia mahindi waliolipia wafanyabiashara hao wa Tanzania jambo hili limeleta mkanganyiko," alisema Mwakajoka.

Alisema walipeleka malalamiko yao kwa Balozi wa Tanzania nchini Zambia ndipo wachache wakapewa lakini hata waliopewa baada ya kupakia mahindi hayo, yalizuiwa njiani katika maeneo ya Kapirimposhi, Mpika, Lusaka na Kasama kabla ya kuyashusha sokoni Nakonde.

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Songwe, Isakwisa Lupembe, alimwomba Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuongeza nguvu kwenye usimamizi wa fedha za umma.



Diwani wa Kata ya Ilolo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, Yohana Mwanjeka, akizindua kitabu cha Tathmini ya Stadi za Maisha na Maadili kwa watoto wenye umri wa kuanzia miaka 13 hadi 17 wilayani humo, (kulia) ni Mjumbe wa Bodi wa Shirika la Elimisha Tanzania, Imelda Ndetewale. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Watoto 400 wapatiwa elimu ya maadili

**Na Grace Mwakalinga,** MBOZI

ZAIDI ya watoto 400 wenye umri wa miaka 13 hadi 17 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, wamepatiwa elimu ya stadi za maisha na maadili kutoka Shirika la Elimisha kwa ufadhili wa Shirika la Milele Zanzibar na Uwezo.

Lengo la kutoa elimu hiyo ni kumsaidia mtoto kukabiliana na vikwazo mbalimbali kwenye maisha, kujitambua, heshima na ushiriki wa shughuli za kijamii kikamilifu.

Mkufunzi wa Mradi Tathmini ya Stadi za Maisha na Maadili katika kaya kutoka Shirika la Uwezo, Anyimike Hezron, alisema hayo juzi alipowasilisha ripoti ya tathmini hiyo baada ya mradi huo kukamilika.

Alisema mradi huo ulitekelezwa katika wilaya 24 nchini na kwamba kwa wilaya ya Mbozi, walivifikia vijiji 20 vyenye watoto 425 na kati yao asilimia 48 ni wasichana na 52 ni wavulana.

"Katika tathmini tuliyoifanya wilayani Mbozi kuhusu stadi za maisha, mtoto mmoja kati ya 10 ana kiwango cha juu cha heshima kwa wengine. Aidha, tulibaini kuwa asilimia 81 ya watoto wako shuleni na asilimia 19 hawako shuleni," alibainisha.

Akizindua ripoti hiyo, Diwani wa Ilolo, Yohana Mwajeka, alisema mradi huo umesaidia kujua matatizo yanayowakabili watoto na namna sahihi ya kuwasaidia ili wakue katika maadili yanayostahili kwenye jamii.

Kuhusu maadili ya watoto, alisema kwa kiwango kikubwa yamepotea kwa sababu ya mtindo wa maisha ya wazazi ambao huchangia watoto kukosa malezi bora.

Alifafanua kuwa idadi kubwa ya wanaume wanachelewa kurudi nyumbani jambo ambalo linachangia kutofuatilia maendeleo ya watoto kielimu na mazingira wanayoishi nyumbani.

"Angalau sasa tathmini hii imetupa picha halisi ya wapi sisi wazazi tunapaswa kusahihisha ili kuokoa kizazi cha watoto wetu, hasa kwenye suala la malezi na maadili. Watoto wanashuhudia migogoro ya baba na mama unadhani wanajifunza nini pindi wanapotengana wazazi zaidi ya kupandikiza chuki na tabia zisizofaa kwa watoto?" Alihoji.

Aliongeza kuwa ripoti hiyo itaisaidia serikali kuona maeneo ya kuboresha, vikwazo na mahitaji ya watoto ili kuwasaidia kwenye ukuaji na kujiamini.

Mfanyakazi kutoka Shirika la Elimisha, Felix Mwakyembe, alisema michango ya wananchi kuhusu tathmini ya ripoti hiyo inachagiza taasisi za kidini, shule na familia kuangalia mambo ya kuyafanya ili kusaidia malezi ya watoto.

Alisema taasisi hizo ni muhimu na zinategemeana katika suala la makuzi na malezi ya watoto ili kuwasaidia kulea katika njia ili sahihi na kuwasaidia kutimiza ndoto zao.

Justina Mwasomola, mkazi wa Ilolo, alisema kuporomoka kwa maadili ya wazazi kumechangia wimbi kubwa la watoto kutokuwa na heshima kwenye jamii.

Alisema kwa sasa wazazi wamejikita zaidi kwenye shughuli za uzalishaji mali kama vile kilimo na biashara na kusahau kufuatilia mienendo ya watoto ambao wakati mwingine wanajifunza tabia mbaya mtaani.





# KMKM yashiriki uchumi wa buluu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum SMZ, Masoud Ali Mohamed, amesema Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimeanza rasmi kutekeleza dhana ya uchumi wa buluu kwa shughuli za ufugaji wa mazao ya baharini wa matango bahari na kuvua samaki aina ya jodari katika maeneo ya bahari kuu.

Masoud alisema hayo Ijumaa wakati akiwasilisha makadirio mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum SMZ kwa mwaka 2023/24 katika Baraza la Wawakilishi, Chukwani.

Alisema KMKM tayari imeanzisha mashamba 17 ya matango bahari katika maeneo ya Unguja na Pemba ikiwa ni kutekeleza dhana ya uchumi wa buluu.

Waziri huyo alisema mashamba 11 yako katika ufukwe wa kambi ya Kibwengo, mkoa wa Kaskazini Unguja katika eneo lenye ukubwa wa eka 11.

Pia alisema mashamba tisa yako katika ukanda wa ufukwe wa kisiwa cha Tumbatu mkoa wa Kaskazini Unguja na mazao hayo tayari yameoteshwa yakiwa katika ustawi mzuri.

"Mheshimiwa Naibu Spika, KMKM tayari inatekeleza dhana ya uchumi wa buluu katika kuanzisha kilimo cha matango bahari jumla ya mashamba 17 ambayo yamestawi vizuri," alisema.

Waziri huyo alisema tayari KMKM kwa kutumia boti za kisasa imeanza kuvua katika eneo la bahari kuu ya ukanda wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuvua samaki aina ya jodari wanaotakiwa kuvuliwa katika maeneo hayo.

Hata hivyo, alisema KMKM imefanikiwa kudhibiti na kupambana na magendo katika maeneo ya pwani ya fukwe za Unguja na Pemba hasa katika maeneo ya bandari bubu.

Alisema vita dhidi ya magendo ni kubwa kutokana na kuwepo kwa wingi wa bandari bubu ambazo zinatumiwa kwa ajili ya kuendesha magendo ambayo huikosesha serikali mapato yake.

Aliitaka Ofisi ya Rais kuongeza bajeti kwa KMKM kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya kufanya doria katika maeneo ya fukwe za Unguja na Pemba kwa kuipatia vifaa vya kisasa.

# Waziri: Mkataba uendeshaji Bandari ya Malindi utaongeza tija na ufanisi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, amesema mkataba wa usimamizi na uendeshaji wa Bandari ya Malindi na Kampuni ya African Global Logistics, utaongeza ufanisi wa utendaji kazi wa bandari hiyo.

Aliyasema hayo kwenye hafla ya utiaji wa saini wa mkataba huo, iliyofanyika huko wizarani kwake Kisauni nje ya mji wa Zanzibar jana.

Dk. Khalid alisema Bandari ya Malindi inakabiliwa na changamoto ya kuzidiwa na utoaji wa huduma hasa za ushushaji na upakuaji wa makontena jambo ambalo linasababisha foleni kubwa ya meli za mizigo.

Alisema serikali baada ya kuliona hilo, iliamua kuchukua jitihada mbalimbali ikiwamo ununuzi wa vifaa, kuweka mifumo ya kisasa na kuongeza nafasi ya kuweka makontena kwenye eneo la Bwawani.

Dk. Khalid alisema hayo yalifanyika katika kuhakikisha bandari inapunguza siku za meli za mizigo kusubiri kufunga na kuongeza gharama ambazo mwananchi ndiye atakayezilipa kupitia huduma wanazozipata. Alisema serikali ilitumia karibu Sh. bilioni 17 kununua vifaa vitakavyosaidia kurahisisha utoaji wa huduma kwenye bandari hiyo, lengo ikiwa ni kurahisisha utoaji wa huduma.

"Ni bandari hiyo iliyojengwa miaka ya 1920, kwa sasa imekosa ufanisi kutokana na ukuaji wa biashara," alisema.

Waziri huyo alisema serikali ya Zanzibar haijabinafsisha Bandari ya Malindi, bali imetiliana saini ya makubaliano ya mkataba wa usimamizi na uendeshaji wa bandari hiyo.

Dk. Khalid, alisema ni matumaini ya serikali kwamba mkataba huo unaongeza wigo wa kiutendaji na kuimarisha utoaji wa huduma, ikizingatiwa uzoefu na utaalamu wa kampuni hiyo.

Naye Mtendaji Mkuu wa African Global Logistics, Tony Sternning, alisema ni matarajio kwa kampuni hiyo kwamba mkataba huo unafikia lengo lililowekwa na pande zote mbili kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar. Aidha, alisema watahakikisha yale yote yaliyoainishwa yanatekelezwa kwa kuongeza ufanisi wa kikazi.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari, Nahmat Mahfoudh, alisema Bandari ya Malindi kwa sasa inakabiliwa na changamoto ya kupokea makontena mengi na makubwa na meli za kisasa kuliko uwezo wa bandari hiyo ambao ujenzi wake hauruhusu kupokea meli na kontena hizo.

Kutokana na changamoto hiyo, alisema serikali imeamua kujenga Bandari ya Mangapwani ili kwenda na mahitaji ya wakati wa sasa kwa kuwa uwezo wake ni kupokea TUS 80,000 lakini bandari mpya itakayojengwa Mangapwani itakuwa na uwezo wa kupokea TUS 800,000 hadi 1,800,000.

"'Kwa hiyo bandari hii itabakia kuwa ya meli za abiria kati ya Zanzibar na Dar es Salaam, kiufupi hii itakuwa bandari ya kitalii", alisema Mkurugenzi huyo.

Mkataba huo uliotiwa saini ni wa miaka matano na utakuwa wa mpito huku malengo yakiwa kukamilisha ujenzi wa bandari ya Mangapwani kwa ajili ya ushushaji na upakizi wa makontena.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja wa Kimataifa wa Benki ya NBC, Wilson Nkuzi, akizungumza na wateja wa benki hiyo (hawapo pichani) jijini Mwanza katika hafla ya utambulisho wa huduma mpya ya kidigitali inayofahamika kama 'NBC Connect' kwa ajili ya wateja wa Kanda ya Ziwa mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkurugenzi ataja siri ongezeko watalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mkuu wa Hoteli ya Sea Clif Zanzibar, Patrick Beck, amesema hali ya amani na utulivu iliyoko nchini imesababisha uingiaji wa watalii wengi Zanzibar na kunufaika kufanya biashara ya kuwahudumia watalii.

Amesema bila ya amani sekta ya utalii ingetetereka na watalii wangeshindwa kufika nchini na maisha ya wananchi yangekuwa magumu.

Aliyasema hayo mwshoni mwa wiki visiwani hapa katika sherehe ya wafanyakazi wa hoteli hiyo ambayo huandaliwa kila mwaka ili kujumuika pamoja na kufanya tathmini ya utendaji kazi. Mkurugenzi huyo alisema taasisi bora hujengwa na wafanyakazi hivyo aliwasisitiza kuendelea kuwa waadilifu katika kazi zao ili kuendelea kupokea watalii wingi.

"Niwaombe mwendelee kuwa waadilifu, wanyenyevu na lugha nzuri ya kuwapokea na kuwahudumia watalii wanaofika hotelini hapa ili kuendelea kutuamini na kumiminika kwa wingi," alisema.

Aidha, alisema hoteli hiyo ni muumini wa ulipaji wa kodi kwa sababu kodi ndiyo inayoiwezesha serikali kufanya mipango yake ya maendeleo katika kutoa huduma kwa wananchi.

Naye Ofisa Rasilimali Watu wa hoteli hiyo, Bariki Shayo, alisema taasisi yoyote inayotaka kupata mafanikio lazima ijengwe na wafanyakazi bora na wenye sifa, hivyo uamuzi wa hoteli hiyo kuwajali wafanyakazi na kuwaweka pamoja ni jambo zuri linalopaswa kuigwa na taasisi zingine. Alisema uongozi wa hoteli hiyo utahakikisha unaendelea kuwajali wafanyakazi wake na kuendelea kuwapa stahiki zao ili kuendeleza maisha yao.

Wafanyakazi wa hoteli hiyo waliushukuru uongozi wa hoteli kwa uamuzi wao wa kuwawekea pamoja na kubadilishana mawazo na wakuu wao kitendo ambacho kinawapa faraja na ari ya kufanyakazi kwa bidii.




Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Bulandya Elikana (katikati), akimsikiliza Msimamizi wa Kituo cha m-mama katika Hospitali ya Sekou-Toure Mwanza, Pascal John (kushoto), akitoa maelezo wakati wa uzinduzi wa mfumo wa m-mama unaotoa huduma ya usafiri wa dharura kwa wajawazito, waliojifungua na watoto wachanga ili kuokoa vifo vya mama na mtoto. Anayeshuhudia ni Mkurugenzi wa TEHAMA wa Vodacom Tanzania PLC, Athuman Mlinga. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Waandishi wakumbushwa kuepuka kuwa ‘machawa’

**Na Christina Mwakangale**

WAANDISHI wa habari nchini wameonywa kujikita kwenye uandishi usiojenga, kishabiki na kusifiana, badala yake wajikite kuandika taarifa zenye kuibua hoja, kuelimisha na kuleta mabadiliko.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere (MNF), Prof. Francis Matambalya, aliyasema hayo jana, jijini Dar es Salaam, wakati Klabu ya Waandishi wa Habari Dar es Salaam (DCPC), ikiadhimisha mwezi wao wa uhuru na vyombo vya habari.

“Kwa kizazi hiki kuna uandishi wa kishabiki, naona mnaita sijui uchawa. Yaani waandishi wapo tayari kujipinda kupika habari, waoga sio majasiri na wapo waandishi wa habari ambao wana unafiki, unaoendana na uoga.

“Ukiangalia uandishi mwingi wa habari za Tanzania ni za kusifiwa. Yaani mnapita mle mle kwenye kauli za kisiasa. Usipokosoa unajenga tatizo. Kuna kitabu cha Mwalimu Nyerere ‘Tujisahihishe’ kinaeleza wazi kuhusu hili.”

“Mbona nyumbani kwako unaweza kumwadhibu mwanao anapokosea, sembuse mtu kiongozi uliyempa dhamana kubwa kuongoza watu. Lazima kukosoa, ili tijisahihishe,” alisema Prof. Matambalya.

Mbali na hilo, Prof. Matambalya alisema fani hiyo iheshimiwe na iwezeshwe kwa kuwa ndiyo taaluma pekee inayobeba uelewa mtambuka kwenye jamii na mwalimu kwenye maeneo yote.

“Waandishi wanabeba mzigo mtambuka ambao unajumuisha mambo muhimu, ikiwamo ualimu kwa maana ya kuelimisha kusahihisha, kujenga uelewa na taswira. Mwandishi wajibu wake ni kuendesha mdahalo wa kitaifa kila siku na mshiriki wa moja kwa moja kuwapatia wananchi matukio yanayoendelea muda wowote.

“Ipo haja ya waandishi kuwa na eneo maalumu la uandishi, ili kujenga uzoefu na ubobevu katika sekta tofauti kama vile afya, uchumi, siasa na elimu,” alisema Prof. Matambalya.

Kadhalika, alitoa wito wa wanahabari kuwa wazalendo kwani ni kiungo muhimu cha kukutanisha wadau wa ndani na nje ya nchi, hivyo ujumbe wa mwandishi ni muhimu na unaohitaji kusimamia haki na usawa.

Alitaja changamoto zilizoko kwenye fani hiyo, zikiwamo mazingira duni ya kazi, na kurudisha nyuma uhuru wa habari ikiwamo rushwa, huku baadhi ya maudhui yanayobebwa kuwa ya nje ya nchi ambayo kati yake huenda kinyume na mila, utamaduni wa Kitanzania.

Mshauri Mwandamizi wa Masuala ya Jinsia na Afya ya Jamii, Dk. Katanta Simwanza, akitoa mada kuhusu kujitambua alisema uelewa duni na kutojitambua ni kati ya changamoto zilizo nyingi kwenye jamii.

Alisema ni muhimu jamii kushirikishwa kwenye masuala mbalimbali na kuzingatia jinsi kwa kuwa kila moja inawakilisha inakiishi, hivyo ushiriki huo utakuwa na uamuzi wenye usawa.

Awali, Mwenyekiti wa DCPC, Samson Kamalamo, alisema kuadhimisha Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani (WPFD), kunatokana na azimio la Umoja wa Mataifa (UN), kuhusu uhuru wa habari duniani.

“Kuunda mustakabali wa haki, uhuru wa kujieleza kama kichocheo cha haki nyingine zote za binadamu’ ni kauli mbinu ya maadhimisho hivyo, tunatoa wito kwa mamlaka zinazohusika na wanahabari, kuziainisha changamoto na kuzitafutia ufumbuzi,” alisema Kamalamo.

Aidha, alizitaja changamoto zilizopo DCPC ikiwamo ukosefu wa vitendea kazi, kama kompyuta ambavyo vitasaidia utendaji kazi katika kipindi hiki ambacho teknolojia imekua na dunia imejikita katika digitali.

## Serikali kuendelea kujenga mazingira wezeshi uwekezaji

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema itaendelea kutengeneza mazingira wezeshi kwa wawekezaji waliopo kwenye mnyororo wa sekta ya nyumba ili kuongeza thamani zaidi.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Kamishna wa Usimamizi wa Deni la Taifa, Japhet Justin, kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, katika hafla ya kuorodheshwa kwa toleo la nne la hatifungani ya Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Tanzania (TMRC) katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Alisema anaamini kuendelea kuiwezesha sekta hiyo ni fursa nzuri ya watu wengi kuingia kuwekeza huko na hata wengine kupata mikopo ya kujenga nyumba zao kwa kutumia mfumo huo ambao ni rafiki kutokana na kutoa muda rafiki wa kulipa.

“Na hatua hii inakwenda kutoa nafasi zaidi ya kuongeza ushawishi kwa watu wengi zaidi kuingia katika mfumo kama huu wa kuorodhesha wenzao katika soko la hisa Dar es Salaam, niwapongeze TMRC kwa hatua hiyo kubwa kwa kuangali fursa ya kuinua soko letu la nyumba na hawaishii katika njia ya kutafuta mikopo ya muda mrefu, lakini pia kutumia Soko la Hisa la Dar es Salaam kama sehemu muhimu kupata mtaji wa hatifungani,”alisema Justin.

“TMRC wanastahili kupongezwa kwa kuwa na mwendelezo, mara nyingi tunafanya mara moja lakini wao wameendelea kubaki kwenye malengo yao na kwa hatua hii wanashawishi wengine kuona fursa hii kubwa.”

“Kwa hiyo imefika wakati tuwaambie watu kwamba wanaweza kujenga nyumba siyo tu mpaka wawe na fedha yao wenyewe, lakini wakati mwingine wanaweza kujenga nyumba kwa kutumia benki kwa kupata mkopo unaoanzia asilimia 13 mpaka 17 wakalipa kwa miaka kati ya 15 hadi 20, wakajenga nyumba zao kwa utulivu na kulipa kidogo kidogo badala ya kukopa kwa mtu binafsi.”

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TMRC, Oscar Mgaya, alisema katika toleo hilo la nne wamefanikiwa kupata wawekezaji zaidi tofauti na walivyokuwa wamepanga.

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha MJINI Mkoa MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 43 /2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**BILAZI KIVIZA MBALE WA NUNGE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA MRISHO BILAZI KIVIZA**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **26 Mwezi 05 Mwaka 2023.** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kama yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
* Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia * Futa isiyohusika
Imetolewa leo tarehe **19 Mwezi wa 05 Mwaka 2023.**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**
**SHAURI LA RUFAA NO. 25 YA 2023**
**MASUMBUKO B. MACHELE..................MDAI**
**DHIDI YA**
**NACHIRO MGENIWARU.....................MDAIWA**
**KWA;**
**NACHIRO MGENIWARU**
**UKEREWE-MWANZA.**
**AU POPOTE ALIPO TANZANIA BARA**
**KUITWA SHAURI**

Kwa kuwa mdai amefungua shauri la madai katika Mahakama ya Hakimu Mkazi MWANZA na kesi imepangwa kutajwa mbele ya Mhe, A.P S SHAO, PRM (Ext. J) tarehe 30 mwezi 05, 2023.
Hivyo basi unatakiwa kuhudhuria bila kukosa au mwakilishi wako ili kusikiliza kesi tajwa hapo juu.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 19 mwezi May, 2023.

HAKIMU MKAZI
MWANZA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo KIHONDA**
**Wilaya ya MOROGORO**
**Mkoa wa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. .2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**NESTOR PAULO SENGO WA KAMBI TANO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA MARTHA OMARY MYOWELA**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 12 Mwezi 05 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa
Imetolewa leo tarehe 5 mwezi 05 mwaka 2023

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA
MOROGORO
HAKIMU

**FOMU MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na 744/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU KAKUBHAI MANJI SAUJANI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA**
**NA RAJEN SHANTILAL VITHLANI**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 5 mwezi 6 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa
**Imetolewa leo tarehe 18 Mwezi wa 5 mwaka 2023**

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**REHEMA ABDUL MALONGO**

anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 971 CFC** aina ya Boxer. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CHU/RB/497038/2022.**

HABARI KIMATAIFA

# Viongozi G7 waionya China kujitanua kijeshi

**HIROSHIMA,** Japan

VIONGOZI wa kundi la Umoja wa Mataifa Tajiri G7 wameionya China dhidi ya kutanua shughuli zake za kijeshi kwenye kanda ya Asia na Pasifiki, licha ya kusisitiza dhamira yao ya kuwa na mahusiano imara na taifa hilo.

Kundi la G7 linaundwa na mataifa ya Japan, Marekani, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Canada na Italia, bila kuusahau Umoja wa Ulaya.

**Kundi la G7 linaundwa na mataifa ya Japan, Marekani, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Canada na Italia, bila kuusahau Umoja wa Ulaya.**

Kwenye tamko la mwisho lililotolewa baada ya mkutano wa kilele wa kundi la G7 uliofanyika mjini Hiroshima nchini Japan, viongozi wa mataifa hayo waliorodhesha masuala kadhaa yanayowatia wasiwasi kutokana na shughuli za kijeshi na kiuchumi za China.

Viongozi hao walitahadharisha dhidi ya kujitanua kijeshi kwa China kwenye eneo la bahari ya kusini na kurejea msimamo wao kwamba amani na uthabiti kwenye ubia wa bahari ya Taiwan ni suala muhimu kwa usalama wa dunia.

Walisema wako tayari kushirikiana na Beijing na kwamba msimamo wanaochukua haulengi kuidhuru China wala kulemaza maendeleo ya kiuchumi ya taifa hilo.

Tamko la pamoja la G7 liliitaka pia China iishinikize Russia kuacha uchokozi wa kijeshi na iviondoe vikosi vyake Ukraine mara moja. Kupitia tamko hilo viongozi wa G7 wameihimiza China iunge mkono amani ya kudumu na haki kwa kuzingatia uadilifu wa kieneo, kanuni na makusudi ya mkataba wa Umoja wa Mataifa (UN), ikiwamo mazungumzo ya moja kwa moja na Ukraine.

Wakitoa wito wa kufanya kazi pamoja katika changamoto zinazoikabili dunia kama vile mabadiliko ya tabia nchi, madeni, mahitaji ya ufadhili wa kifedha kwa mataifa masikini, masuala ya afya yanayohusu dunia na uthabiti wa kiuchumi, viongozi wa kundi hilo la mataifa saba tajiri duniani wamesema, ushirikiano na China unahitajika kutokana na nafasi ya taifa hilo duniani na kiuchumi.

Hata hivyo, viongozi hao wametahadharisha pia nchi zinazojaribu kutumia biashara kama silaha na kusema kuwa zitakabiliwa... kauli ambayo imeipa China ishara kuhusu mienendo ambayo Marekani inasema ni uonevu wa kiuchumi.

G7 kwa kauli moja imeonyesha wasiwasi kuhusu hali ya haki za binadamu nchini China hasa katika majimbo ya Tibet, Hong Kong na Xijiang ambako watu wengi wanakabiliwa na tatizo la kushurutishwa kufanya kazi.

Wakati huohuo, Rais wa Ukraine Volodymyr amepeleka wito wake wa kutaka kuungwa mkono dhidi ya Russia kwenye mkutano wa G7, na kwamba alifika Hiroshima ikiwa ni muda mfupi baada ya Ikulu ya Marekani kutangaza uamuzi iliyouita wa kihistoria wa kuipatia Ukraine ndege za kivita chapa F 16.

Wakati alipowasili mapema jana mjini Hiroshima Zelensky alisema kuwa mkutano wa G7 ungeongeza ushirikiano utakaoipa ushindi Ukraine. **DW**



Viongozi wa Jumuiya la Mataifa Tajiri G7, mashirika ya kimataifa na washirika wakiwa katika mkutano wa kilele cha jumuiya hiyo uliotamatika jana nchini Japan. **PICHA: MTANDAO**

# Polisi yakabiliana na waandamanaji DRC

**KINSHASA,** DRC

POLISI nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) wametumia gesi ya kutoa machozi ili kuwatawanya waandamanaji katika mji mkuu Kinshasa, baada ya viongozi wa upinzani kuitisha maandamano kama njia ya kuipinga serikali.

Inaelezwa kuwa viongozi wa upinzani walioitisha maandano hayo mwishoni mwa wiki iliyopita ni aliyekuwa Waziri Mkuu Matata Ponyo, Martin Fayulu, Moise Katumbi na Delly Sesanga, na kwa walitekeleza jambo hilo kwa nia ya kukemea gharama ya juu ya maisha, ukosefu wa usalama Mashariki mwa DRC na hali ya kutoweka wazi katika maandalizi ya uchaguzi uliopangwa kufanyika mwishoni mwa mwaka huu.

Ilibainishwa kuwa majadiliano yalikumbwa na vurugu pale wafuasi wa upinzani walipokataa kufuata mwongozo uliowekwa na serikali wakisema kuwa si wa haki na unalenga kuwazuia ili wasiandamane.

Martin Fayulu, alisema kuwa hali ya polisi kutawanya wanaoandamana inadhihirisha wazi kwamba serikali ya Felix Tshisekedi imeshindwa kutekeleza sera yake ya kukuza haki na sheria kama inavyosema katiba ya nchi, huku wakitumia lawama polisi kwa kushindwa kutekeleza majukumu yao.

Gavana wa mkoa wa Kinshasa, Gentini Ngobila pia alilaumu upinzani kwa kuitisha maandamano yaliyosababisha vurugu na kuhatarisha usalama wa umma.

Pia ilielezwa kuwa katika purukushani hizo zaidi ya watu saba walijeruhiwa wakiwamo askari polisi watu pamoja na waandamanaji. Na kwamba hakujatolewa tamko lolote kutoka kwa serikali. **VOA**

# Ubalozi wa Qatar washambuliwa



**KHARTOUM,** Sudan

UBALOZI wa Qatar umevamiwa na kushambuliwa na watu wenye silaha kutokana na machafuko yanayoendelea mjini Khartoum nchini Sudan, jambo linaloonyesha kuendelea kwa machafuko ambayo yanatawala taifa hilo kwa zaidi ya mwezi mmoja sasa.

Wakazi wa Khartoum waliliambia shirika la habari la (AFP) jana, kwamba mashambulizi ya anga yanayozidi kufanyika yanasababisha hadi kuta za nyumba kutikisika, jambo ambalo linazidi kuhatarisha usalama wao.

Kwa kupuuza wito wa kusitishwa mapigano, jeshi, linaloongozwa na Jenerali Abdel al-Burhane, na wanamgambo wa Kikosi cha Msaada wa Haraka (RSF) cha Jenerali Mohamed Daglo, wanagombana kwa udhibiti wa maeneo ya kimkakati na madaraka.

Mashuhuda walieleza kuwa mashambulizi yalifanyika karibu na makao makuu ya televisheni ya umma, huku pande zote mbili zikiendelea kudai ushindi kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari.

Tangu kuanza kwa mapigano Aprili 15, mwaka huu, mapigano hayo yamesababisha karibu watu 1,000 kupoteza maisha na zaidi ya milioni moja kuyahama makazi yao na wengine kukimbilia katika nchi jirani.

Wakati mazungumzo ya mapatano ya kibinadamu yakikwama, Jenerali Burhane aliwateua wafuasi wake watatu waaminifu kwenye uongozi wa jeshi na kumfukuza kazi Jenerali Daglo kutoka wadhifa wake kama naibu wa Baraza la Utawala siku ya Ijumaa na kumteua Malik Agar katika nafasi yake.

Aidha, ilielezwa kuwa muasi huyo wa zamani ambaye alitia saini makubaliano ya amani na mamlaka ya Khartoum mwaka 2020 amlitangaza mwishoni mwa juma lililopita kwamba anataka kusitisha vita na kuketi kwenye meza ya mazungumzo.

"Utulivu wa Sudan unaweza tu kurejeshwa na jeshi lenye weledi na umoja," alisema.

Mapambano kati ya watu hao wawili kugombea madaraka yamehatarisha usalama wa wananchi, kuharibu miundombinu ikiwamo makazi na kuiingiza Sudan si tu katika machafuko, bali na kulididimiza kiuchumi. **RFI**

# YANGA YASABABISHA RATIBA LIGI KUU BARA KUBADILISHWA

Na Adam Fungamwango

USHIRIKI wa klabu ya Yanga kwenye michuano ya kimataifa ikiwa ni timu pekee iliyobaki nchini, imesababisha kubadilishwa kwa ratiba ya Ligi Kuu ambapo sasa mechi za mwisho kumalizia msimu zitachezwa Juni 9, badala ya Mei 28 kama ilivyokuwa awali.

Taarifa iliyotolewa jana na Bodi ya Ligi chini ya Idara ya Habari na Mawasiliano, imesema sambamba na mabadiliko ya raundi hiyo ya 30, pia raundi ya 29 nayo imepangwa kucheza Juni 6, mwaka huu, badala ya Mei 24 kama ilivyopangwa awali.

**Bodi imesema imelazimika kufanya hivyo ili kutoa nafasi kwa klabu ya Yanga kucheza michezo yake mwili ya fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika Mei 28 hapa nyumbani na Juni 3 nchini Algeria dhidi ya USM Alger.**

Imesema imeamua kufanya mabadiliko hayo baada ya majadiliano ya ndani yanayojikita kuhakikisha uwepo wa haki na usawa michezoni na kuondoa uwezekano wa upangwaji wa matokeo kama wataachia timu zingine ziendelee kucheza na zingine zisubiri.

"Bodi ya Ligi Kuu ya Tanzania (TPLB) inawataarifu kuwa timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu msimu wa 2022/23 zitacheza michezo yao ya mwisho raundi ya 30, Juni 9, mwaka huu ili kutoa nafasi kwa Yanga kucheza michezo yake ya fainali ya Kombe la Shirikisho," ilisema sehamu ya taarifa hiyo ya Bodi.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotumwa kwa klabu hivi karibuni na kutangazwa kwa umma jana (juzi), michezo ya mwisho ya timu zote ukiondoa Yanga dhidi ya Prisons ilipangwa kufanyika Mei 28, lakini Bodi imelazimika kufanya mabadiliko hayo ili kuhakikisha uwepo na haki na usawa michezoni kuondoa mazingira ya upangaji wa matokeo.

Kwa mantiki hiyo, msimu wa Ligi Kuu 2022/2023 utafikia tamati Juni 9 kwa michezo hiyo ya mwisho.



Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko wa Kampuni ya kubashiri michezo ya Meridianbet Tanzania, Matina Nkurlu (wa pili kulia), akishiriki kugawa viakisi mwanga 'reflector' kwa madereva wa bodaboda Mbagala jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ruvu Shooting yawaomba radhi mashabiki

Na Shufaa Lyimo

UONGOZI wa klabu ya soka ya Ruvu Shooting umewaangukia mashabiki na kuwaomba radhi kufuatia timu hiyo kushuka daraja msimu huu.

Msemaji wa klabu hiyo, Masau Bwire, amesema kushuka daraja kwa timu hiyo kumewaumiza na kuwaomba radhi mashabiki wa timu hiyo ambao wamekuwa wakiisapoti muda wote.

Bwire aliweka wazi kuwa wadau wengi wa mpira wa miguu nchini walitamani timu hiyo iendelee kushiriki kubaki Ligi Kuu Tanzania Bara huku wakitarajia makubwa msimu ujao.

"Kwanza ninawaomba radhi wapenzi wa Ruvu Shooting na Watanzania kwa sisi kushuka daraja, naamini wengi wao walikuwa wanatamani kuona timu yetu inaendelea msimu ujao," alisema Bwire.

Alisema amepokea kwa mikono miwili kile kilichowakumba msimu huu na kudai wanakwenda kuiamsha Ligi daraja la kwanza ambayo kwa sasa imepoteza msisimko.

"Tunajiandaa na ligi daraja la kwanza ambayo imepoteza msisimko, tunataka tuwaonyeshe sisi ni nani ili msimu ujao turudi tunakostahili kuwapo, yaani kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema Bwire.

Aidha alisema baada ya kumaliza michezo yao miwili iliyobakia msimu huu moja kwa moja wataanza maandalizi ya Ligi daraja la kwanza.

"Tunaomba mashabiki pamoja na wadau wetu waendelee kutupa ushirikiano kwani naamini tutarejea kwenye ligi na tutarejea kwa kishindo," alisema msemaji huyo.

## Pius Mpenda amtwanga Mmoroco kwa KO Dubai

NNa Saada Akida

BINGWA wa mkanda wa WBU katika uzani wa Super Middle, Mtanzania, Pius Mpenda, jana alifanikiwa kumtwanga kwa KO katika raundi ya nane Moughit El Moutaoaukil wa Morocco katika pambano lililopigwa jana Dubai.

Mpenda ameshinda pambano hilo lililopigwa kwenye ukumbi wa EMD Fitnes Center likiwa la raundi nane katika uzani wa 'Middle'.

Mtanzania huyo kutoka 'Naccoz Camp' anaendeleza rekodi yake ya kuendelea kushinda mapambano yake ya nje baada ya Desemba mwaka jana kufanikiwa kushinda ubingwa wa WBU nchini Uganda kwa kumchapa Faruk Daku raia wa nchi hiyo.

Mpenda ameweka rekodi mpya ya kuwa bondia wa kwanza wa Tanzania kushinda pambano la kimataifa nje ya mipaka ya Tanzania tangu kuingia kwa uongozi mpya wa Kamisheni ya Ngumi za kulipwa nchini TPBRC chini ya Chaurembo Palasa.

Mbali ya Mpenda, Watanzania wengine wawili walipanda ulingoni kwenye pambano hilo lililoandaliwa na Promota Eisa El Dah, Mwinyi Mzengela aliyepoteza mbele ya Sahel Afridi raia wa Saudi Arabia wakati Safarina Bela akipoteza dhidi ya Asha Roka wa India.

## Meridianbet Tanzania yawageukia bodaboda

Na Saada Akida

MKUU wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko wa Kampuni ya Meridianbet Tanzania, Matina Nkurlu, amesema kupitia mchezo wa kubashiri kampuni hiyo haijawaacha nyuma madereva wa bodaboda baada ya kuwaletea mchezo mpya wa "CHAGUA TUKUPE".

Akizungumza na Nipashe jana baada ya kutoa zawadi ya 'Reflectors' kwa waendesha bodaboda wa Mbagala jijini Dar es Salaam, Nkurlu alisema ni utaratibu wa Meridianbet wa kurudisha kwa jamii kila inapopata fursa ya kufanya hivyo.

Alisema kuigusa jamii kwa namna moja ama nyingine ni kuwafikia na kuwapa misaada mbalimbali inayohitajika kwa wakati husika.

Alisema wameamua kuwapatia "Reflectors' hizo ili ziwasaidie kwenye shughuli zao za kila siku za kutafuta riziki.

"Huu utakuwa mwendelezo wa kutoa vifaa vitakavyowasaidia bodaboda katika shughuli za kila siku huku tukiwaletea mchezo mpya wa 'Chagua Tukupe', katika kubashiri mechi mbalimbali ikiwamo ile ya EPL, La Liga, Serie A na Bundersliga pamoja ligi zingine nyingi lakini kuna michezo ya Avaitor, Sloti, Poker, Roulette na mingine ambayo itakuwa rahisi kwa watu kupiga mkwanja," alisema Nkurlu.

Aliongeza kuwa Meridianbet imeleta pia utaratibu wa bonasi ya ukaribisho kwa wateja wapya ambapo wote watapa kianzio cha kucheza michezo ya Kasino.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ALIISTER AKARIBIA LIVER

LIVERPOOL inakaribia kufikia kabisa makubaliano ya kumsajili kiungo wa kati wa Briton, Alexis Mac Allister, 24, ingawa bado hawajasaini mkataba. ***(Fabrizio Romano)***

### MITOMA KUZUIWA

KOCHA wa Brighton, Roberto de Zerbi ameiambia bodi ya klabu hiyo izuie kila dau kwa ajili ya winga wao Mjapan Kaoru Mitoma, 26, huku Mac Allister na kiungo wa kati wa Equador, Moises Caicedo, 21, wakiwa tayari wanajiandaa kuondoka Seagulls. ***(Football Insider)***

### KIMMICH AWINDWA

ARSENAL, Liverpool na Barcelona zina nia ya kumnunua kiungo wa kati wa Bayern Munich na Ujerumani, Joshua Kimmich, 28. ***(Marca)***

### GUNDOGAN MKATABA MPYA

MANCHESTER City itatoa ofa kwa kiungo wa kati wa Ujerumani, Ilkay Gundogan, 32, ya mkataba mpya hadi Juni 2024, huku Barcelona wakiwa na nia naye. ***(Fabrizio Romano)***

### MOYES KUONDOKA

KOCHA wa West Ham, David Moyes anapanga kuondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu. ***(Football Insider)***

### CANCELO AWINDWA BARCA

KIUNGO wa Manchester City na Ureno, Joao Cancelo, 28, anafuatiliwa kwa karibu na Barcelona, huku Bayern Munich ikiwa haina uwezekano kabisa wa kurefusha zaidi mkataba wa mkopo na mchezaji huyo. ***(Mundo Deportivo)***

### AWANIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United iko mbele katika kinyang'anyiro cha kuwania saini ya mlinzi wa Arsenal na Scotland, Kieran Tierney mwenye umri wa miaka 25 msimu huu, huku Manchester City na Aston Villa pia wakimtaka. ***(Football Insider)***

### RAYA ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA inataka kumsajili mlinda mlango wa Brentford na Hispania, David Raya, 27, ambaye anathaminishwa kwa karibu pauni milioni 40. ***(Givemesport)***

### SCAMACCA KUACHIWA

WEST Ham iko tayari kumuacha mshambuliaji, Gianluca Scamacca wa Italia arejee kwenye Ligi Kuu ya Serie A mwaka mmoja tu baada ya kujiunga na Sassuolo, huku AC Milan wakimfuatilia kwa karibu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Gazzetta dello Sport)***

### KIM SAFI PSG

MLINZI wa kati wa Korea Kusini, Kim Min-jae, 26, amefanya mazungumzo ya awali na Paris St-Germain, huku miamba hiyo ya Ufaransa ikiungana na Manchester United katika kinyang'anyiro cha kumwania beki huyo wa Napoli. ***(Mirror)***

### ORBAN AGOMBEWA EPL

MANCHESTER United na Chelsea zipo kweye mbio moja kuwania kupata huduma ya mshambuliaji wa Gent na Nigeria, Gift Orban, 20. ***(FourFourTwo)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA ASHUKURU MASHABIKI, MAN CITY IKIBEBA KOMBE LA TANO

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City imeshinda taji lao la tano la Ligi Kuu ya England ndani ya misimu sita baada ya Arsenal kufungwa 1-0 na Nottingham Forest Jumamosi, huku Kocha Pep Guardiola akisema mashabiki wao ndio chachu kubwa.

**Kufungwa kwa Washikabunduki hao walionyuma ya Man City kwa pointi nne kwenye msimamo wa Ligi huku wakiwa wamebakiwa na mchezo mmoja pekee kuchezwa, kulimaanisha kuwazawadia taji hilo.**

Vijana wa Guardiola walitumia muda mwingi wa msimu huu kuwawinda Arsenal, na walipata nafasi nzuri zaidi bada ya ushindi wao wa 4-1 kule Etihad mwezi uliopita.

Nyota wa Norway, Erling Haaland, ambaye alivunja rekodi ya mabao kwenye ligi hiyo, aliwafanya City kuwa kileleni, huku pia wakiwania kutwaa mataji mengine mawili msimu huu (FA na Ligi ya Mabingwa Ulaya) ambapo yote wametinga fainali.

**●●● Kila siku wanasaidia kutupatia wachezaji na chochote tunachohitaji ili kujaribu...**

Guardiola alizungumzia kuungwa mkono na mashabiki wao kuwa moja ya sababu ya kuamua ushindi wao msimu huu.

Alisema: "Mashabiki wetu wa ajabu wamekuwa nasi kila hatua kwenye safari hii. Bila msaada wao wa ajabu sidhani kama kuna njia yoyote ambayo tungeweza kufikia kile tumefanya misimu sita iliyopita.

"Shauku na uungwaji mkono wao imekuwa muhimu sana na ya kutia moyo kwetu sote. Tunatumaini kushinda taji la Ligi Kuu tena ni njia muafaka kwetu kusema asante kwa mashabiki wetu."

Naye nahodha wa Man City, Ilkay Gundogan alikuwa mtu muhimu sana wakati wa kinyang'anyiro cha timu yake na aliipongeza timu nzima nyuma ya kunyakua taji la tatu mfululizo.

Alisema: "Kuisaidia Klabu kushinda taji la tatu mfululizo la Ligi Kuu ni jambo la kipekee sana.

"Ligi Kuu England bila shaka ndiyo yenye ushindani mkubwa duniani hivyo inakuambia kila kitu kuhusu mafanikio haya.

"Pia ningependa kumshukuru Pep, wafanyakazi wote na kila mtu anayefanya kazi katika klabu hii ya soka.

"Kila siku wanasaidia kutupatia wachezaji kila kitu tunachohitaji ili kujaribu kupata mafanikio.

"Kushinda kombe hili mara tatu mfululizo na mara tano katika miaka sita ni jambo la kushangaza. Ubora huo na uthabiti husaidia kuhitimisha kile ambacho Manchester City inasimamia na kuhakikisha Klabu itaendelea kujitahidi kupata mafanikio ya kusonga mbele.

"Umekuwa msimu ambao sitausahau kamwe."


SportPesa
LIVE IN PLA

MECHI KALI
NEWCASTLE
VERSUS
LEICESTER
1 | 1.34
X | 5.02
2 | 6.82

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP SASA KUKOMAA NA LIGI YA EUROPA



**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amekubali kushindwa katika mbio za kuwania nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa baada ya timu yake kutoka sare ya 1-1 na Aston Villa Jumamosi, akisema hawajaharibika sana na kufurahia Ligi ya Europa msimu ujao.

Baada ya kuangusha pointi mbili kwenye uwanja wa Anfield, Liverpool wanahitaji kushinda mchezo wao wa mwisho dhidi ya Southampton, na wanapaswa kuombea Manchester United au Newcastle United kutopata pointi hata moja katika mechi mbili walizosalia nazo.

"Tutaifanya Ligi ya Europa kuwa shindano letu," alisema Klopp akiiambia BBC Sport.

"Sijakosea kiasi hicho. Kwamba tayari tumefuzu kwa Ligi ya Europa ni jambo la kushangaza kwa timu hizi zote zinazotuzunguka. Hiyo ni ngumu sana na tulifanya hivyo, ni nzuri.

"Kwa muda mrefu hatukuweza hata kusikia sauti ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, hivyo ndivyo tulivyokuwa mbali. Ligi ya Ulaya iko sawa kabisa. Hebu tuone tunachoweza kufanya."

Jacob Ramsey aliifungia Villa bao la kuongoza katika kipindi cha kwanza na wakaweza kuwaweka pembeni wenyeji kwa muda mwingi wa mechi.

Hata hivyo, umati wa watu wa Anfield ulilipuka pale Mbrazil Roberto Firmino alipotoka kwenye benchi na kufunga bao la kusawazisha dakika ya 89 katika mechi yake ya mwisho ya nyumbani akiwa na Liverpool baada ya misimu nane ya kukaa hapo.

Liverpool hawakuweza kupata ushindi wa kuchelewa zaidi, lakini Klopp alisema ameridhishwa na matokeo kutokana na timu yake ilivyokuwa wiki chache zilizopita.

"Ni sare na ni sawa," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari.

## Arteta: Inaumiza kulikosa taji EPI



**LONDON,** England

MIKEL Arteta ameitaka Arsenal kuimarika kama timu baada ya kuipa Manchester City ubingwa wa Ligi Kuu ya England Jumamosi kwa kuchapwa 1-0 na Nottingham Forest.

Kikosi cha Pep Guardiola kilitawazwa mabingwa bila kucheza baada ya bao la Taiwo Awoniyi dakika ya 19 likitosha kuwapa Forest ushindi muhimu uliowahakikishia nafasi yao kwenye Ligi Kuu kwa msimu mwingine.

Arsenal waliongoza kwa tofauti ya pointi nane mwanzoni mwa Aprili lakini mfululizo wa ushindi mara mbili katika mechi nane uliwafanya wasalimu amri na kuwapa City faida wakati wakishinda mechi 11 mfululizo.

Arteta alisema: "Sasa lazima tupone. Inauma sana. Ni lazima nitafute njia ya kuwainua wachezaji na tuna wiki ngumu mbele yetu.

"Ni siku ya huzuni sana. Hisia nyingi ngumu. Tulipoteza mchezo na tukapoteza ubingwa baada ya miezi 10 na nusu kuupigania na miezi tisa na nusu kuwa karibu kabisa na ubingwa.

"Tulijenga hamasa na imani kubwa kuwa tunawe-
za kufika mbali na kus
inda, mwisho tukashindw
kwanza niwapongeze Ma
City, ni mabingwa na wana
tahili kuwa mabingwa.

"Hatujaweza kufany
hivyo. Kwa upande wang
naomba radhi kwa sabab
tumejenga imani kwamb
tunaweza kufanya hivyo n
mwisho timu haikuwez
Hilo ni jukumu langu.

Alipoulizwa kubainisha
wapi taji lilipotoka kutol
kwa uwezo wao, Arteta a
taja sare za mwezi uliopi
dhidi ya Liverpool na We
Ham walipoongoza 2-0 k
tika michezo yote miwili n
kumaliza 2-2.

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# POLISI YAAHIDI 'KUZIKABA' SIMBA, AZAM LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Polisi Tanzania imesema haitokubali kushuka daraja kinyonge, badala yake inataka kuzing'ang'ania Simba na Azam kwa kushinda mechi hizo kujiweka katika nafasi ya kwenda kwenye hatua ya 'play off'.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, John Tamba, amesema wanatambua presha walionayo mashabiki wa timu hiyo, lakini wamejiandaa vizuri kumalizika mechi mbili zilizobaki kwa ushindi ili kujiepusha kwenye janga la kushuka daraja.

"Tunaendelea na mazoezi yetu kwenye uwanja wa Chuo cha Polisi Moshi, tumejipanga vizuri kumalizia mechi zetu mbili, tunajua hatuko kwenye nafasi nzuri sana, lakini tukishinda mechi zetu mbili tunaweza kuepuka kushuka daraja, tunakwenda kucheza dhidi ya Simba na mwisho Azam, ni mechi ngumu na kubwa, lakini tumejiandaa kwa kila kitu na tunaendelea kuwaandaa wachezaji kimwili na kiakili kwa ajili ya kupambana," alisema Tamba.

**Kwa mujibu wa ratiba mpya, Polisi Tanzania itacheza dhidi ya Simba Juni 6 kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi na pia itamalizia mechi zake msimu huu kwenye uwanja huo huo dhidi ya Azam FC, Juni 9.**

Timu hiyo ipo kwenye hatari zaidi ya kushuka daraja kuliko timu nyingine yoyote baada ya Ruvu Shooting kutangulia.

Polisi inashika nafasi ya 15, ikiwa na pointi 25, lakini ikisalia na mechi hizo ngumu na kama ikishinda itafikisha pointi 31, huku ikiombea timu za Mtibwa Sugar na KMC zipoteze mechi zao mbili kwani zote hizo zina pointi 29.

Timu hizo mbili zikishinda mechi moja tu zitafikisha pointi 32 na moja kwa moja itakuwa ni tiketi kwa Polisi Tanzania kushuka daraja.

## Viongozi Simba waingia 'msituni'

INATOKA UK. 23

gumzo ambayo kama yakienda vizuri watamalizana nao na wanaamini ubora wa wachezaji wao lakini maboresho makubwa yanahitaji katika kuelekea usajili wa msimu ujao.

"Viongozi wako makini na tayari wako msituni kwa ajili ya kuanza kuangalia aina ya wachezaji aliopendekeza kocha Robertinho ikiwamo wachezaji aliomba asajiliwe kama mshambuliaji mwenye uwezo zaidi ya Jean (Baleke), kiungo mshambuliaji na mkabaji," alisema Ahmed.

"Lengo ni kutengeneza kikosi bora na tishio Afrika na zaidi kufika hatua ya nusu fainali hadi fainali katika michuano ya kimataifa, Robertinho katika kikao ametoa mapendekezo ya kusajiliwa kiungo mshambuliaji mwenye kasi na uwezo mkubwa wa kufunga na kutengeneza mabao kwa wenzake zaidi ya Chama (Clatous), " alisema Meneja huyo wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba.



Wachezaji wa Azam wakiwa kwenye mazoezi jana kujiandaa na mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union utakaochezwa Juni 24, Mkwakwani, Tanga. **PICHA: AZAM FC**

## *Yanga ni Mayele, Mayele ni Yanga*

INATOKA UKURASA 24

Stephane Aziz Ki na kuanza kufanya mashambulizi mfululizo langoni mwa Singida Big Stars lakini safu ya ulinzi ya 'Walimaalizeti' hao ilikuwa imara.

Alikuwa ni Clement Mzize, dakika ya 22, akiwa kwenye wingi ya kushoto, aliwahadaa mabeki wa wenyeji wao, akaingia ndani kidogo na kuachia mkwaju wa juu ambao ulimkuta kipa Benjamin Haule amekaa imara na kuudaka.

Farid Mussa angeweza kuipatia Yanga bao dakika ya 32, lakini wakati akikimbilia pasi ya mwisho iliyopigwa na Mzize, alianguka na ikawa rahisi kwa mabeki wa Singida Big Stars kuuondosha.

Kipa Haule alifanya kazi ya ziada dakika ya 36, alipookoa mara mbili kwa wakati mmoja mashambulizi ya wachezaji wa Yanga, Farid Mussa ambaye alipiga shuti alilolipangua kabla ya kumkuta Azizi Ki aliyeunganisha tena kuelekea golini lakini kipa huyo aliuwahi na kuudaka.

Kazadi Kasengu aliikosesha Singida Big Stars bao la wazi dakika tano kabla ya mapumziko, alipobaki yeye na kipa Metacha, lakini alijichanganya mwenyewe na kupiga mpira hafifu ambao pia ulikwenda nje ya lango, huku kipa akiwa ametoka langoni kumfuata.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko, lakini yale ya dakika ya 70 ya Yanga ndiyo yaliyokuwa na tija kwani wachezaji walioingia waliongeza kasi ya mchezo.

Kitu kilichowaponza zaidi Singida Big Stars, iliamua kurudi nyuma dakika 20 za mwisho na kuwaachia Yanga kuwa na mpira, kitu ambacho kilianza kuwa hatari kwao, huku Tuisila Kisinda, Mayele na Musonda wakiwa mwiba hatari tangu kuingia kwao.

Medie Kagere atajilaumu kwa kushindwa kuisawazishia timu yake dakika za mwisho baada ya shuti lake akiwa na kipa kupanguliwa na kutoka nje.


## MECHI ZA USHINDI

"1" – NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" – NI TIMU KUTOKA SARE
"2" – NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 22/05/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 3537 | Fasil Kenema vs Sidama Bunna SC | 1.99 | 2.94 | 3.87 |
| 15:15 | 3764 | TT Ha Noi vs SHB DA Nang | 1.22 | 5.01 | 11.25 |
| 15:30 | 2469 | Turan Tovuz vs Sabayil | 2.50 | 3.17 | 2.60 |
| 15:30 | 2476 | Sabah vs Zira | 1.44 | 4.15 | 6.02 |
| 15:30 | 4592 | Karabakh vs FK Sumgayit | 1.12 | 7.26 | 14.51 |
| 15:30 | 4744 | Keshla FK vs Gabala | 3.48 | 3.17 | 2.01 |
| 15:45 | 4560 | Ararat Armenia vs Van Yerevan | 1.19 | 5.00 | 9.60 |
| 17:30 | 4008 | Bunyodkor vs Navbahor Namangan | 3.39 | 2.93 | 2.11 |
| 17:30 | 4050 | Valmiera Fk/Bjss vs BFC Daugavpils | 1.42 | 4.44 | 5.78 |
| 17:30 | 5147 | FC Andijon vs Qizilqum | 2.04 | 3.08 | 3.39 |
| 18:00 | 1545 | FC KTP vs Seinajoen JK | 3.54 | 3.29 | 1.91 |
| 18:00 | 1621 | AC Oulu vs Honka | 2.93 | 3.08 | 2.25 |
| 18:00 | 2826 | Haka vs VPS Vaasa | 1.85 | 3.34 | 3.70 |
| 18:00 | 3132 | FK Panevezys B vs FK Minija | 2.57 | 3.14 | 2.49 |
| 18:00 | 4371 | Inter Turku vs IFK Mariehamn | 1.68 | 3.66 | 4.13 |
| 18:00 | 5148 | Wolkite City FC vs Dire Dawa Kenema FC | 2.30 | 3.01 | 3.01 |
| 18:00 | 5306 | Urartu vs Bkma Yerevan | 1.25 | 5.09 | 9.96 |
| 18:30 | 2433 | Hifk vs Japs | 1.86 | 3.39 | 3.60 |
| 19:00 | 1562 | AL Faiha vs Al Raed Club | 2.00 | 3.62 | 3.40 |
| 19:00 | 1675 | P-Iirot vs Grankulla Ifk | 2.05 | 3.58 | 3.01 |
| 19:00 | 1861 | Dhamk vs Abha | 1.94 | 3.62 | 3.62 |
| 19:00 | 2699 | El Ittihad Alexandria vs Al Masry Club | 2.76 | 2.96 | 2.61 |
| 19:00 | 2742 | Radnik Surduluca vs Kolubara | 1.35 | 4.22 | 7.62 |
| 19:00 | 3945 | FK Mladost Gat vs FK Napredak | 1.61 | 3.23 | 5.54 |
| 19:00 | 4005 | Al-Ettifaq vs Al Fateh (KSA) | 2.82 | 3.51 | 2.32 |
| 19:00 | 4587 | East Riffa vs Al Hala Muharraq | 2.09 | 3.21 | 3.21 |
| 19:00 | 4828 | Javor Ivanjica vs Mladost Lucani | 1.98 | 3.08 | 3.55 |
| 19:00 | 4831 | Radnicki Nis vs Spartak Subotica | 1.92 | 3.13 | 3.70 |
| 19:00 | 4962 | Tampereen Ilves 2 vs FC Jazz | 2.84 | 3.88 | 2.04 |
| 19:00 | 5021 | Nizhny Novgorod vs Sochi | 2.61 | 3.14 | 2.58 |
| 19:00 | 5586 | ASEC Mimosas vs Asi D Abengourou | 1.47 | 3.78 | 6.42 |
| 19:00 | 5670 | Chrobry Glogow vs Skra Czestochowa | 2.52 | 3.14 | 2.53 |
| 19:30 | 2966 | Roma vs Salernitana | 1.46 | 4.00 | 6.41 |
| 20:00 | 1453 | Vasteras SK vs Osters IF | 2.23 | 3.41 | 3.04 |
| 20:00 | 2426 | IFK Varnamo vs Kalmar | 2.73 | 3.09 | 2.39 |
| 20:00 | 2635 | Meppen vs Dynamo Dresden | 5.67 | 4.30 | 1.49 |
| 20:00 | 2930 | Tondela vs Porto B | 2.33 | 3.23 | 2.81 |
| 20:00 | 3323 | Warta Poznan vs GKS Piast Gliwice | 2.51 | 3.13 | 2.55 |
| 20:00 | 5109 | Trabzonspor vs Fatih Karagumruk | 1.66 | 3.93 | 4.40 |
| 20:10 | 2491 | Norrkoping vs Elfsborg | 2.83 | 3.29 | 2.21 |
| 21:00 | 3434 | Vestmannaeyjar vs Hafnarfjordur | 2.44 | 3.52 | 2.47 |
| 21:30 | 1544 | Al Taawon vs AL Tai | 1.84 | 3.77 | 3.83 |
| 21:30 | 3312 | Al Wehda vs Al Khaleej Club | 2.17 | 3.45 | 3.13 |
| 21:30 | 4856 | El Daklyeh vs Zamalek | 4.32 | 3.17 | 1.86 |
| 21:30 | 4873 | Arab Contractors vs Talaea El Gaish | 2.14 | 2.86 | 3.72 |
| 21:45 | 2638 | Le Havre vs Valenciennes | 1.54 | 3.71 | 5.81 |
| 21:45 | 3947 | Empoli vs Juventus | 4.60 | 3.50 | 1.70 |
| 22:00 | 1113 | Newcastle vs Leicester | 1.34 | 5.02 | 6.82 |
| 22:15 | 3794 | Fram Reykjavik vs KR Reykjavik | 2.75 | 3.58 | 2.19 |
| 22:15 | 5331 | Stjarnan vs Fylkir | 1.93 | 3.63 | 3.27 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Mei 22, 2023

Nipashe




Klopp kukomaa na Europa

UKURASA 22

# YANGA NI MAYELE, MAYELE NI YANGA

●●● Aingia dakika ya 70 na kuipeleka timu yake fainali kombe la FA, sasa kukutana...

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA hatari wa Yanga, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Fiston Mayele, ameendelea kuonyesha uwezo na umuhimu wake kwenye kikosi cha timu hiyo baada ya jana kutokea benchi dakika ya 70 na kuifungia timu yake bao muhimu dhidi ya Singida Big Stars na kupeleka timu yake fainali ya kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania, TFF (Kombe la FA)

**Ilimchukua mshambuliaji huyo dakika 12 tangu kuingia uwanjani kuiandikia Yanga bao pekee baada ya kuuwahi mpira uliotemwa na golikipa wa Singida Big Stars, Benjamini Haule.**

Bao hilo lilianzia kwenye winga ya kulia kwa Kenedy Musonda ambaye alipiga krosi iliyookolewa na mabeki wa Singida Big Stars, lakini mpira haukwenda mbali, ukakutana na Denis Nkane ambaye aliachia shuti kali la karibu lililopanguliwa na kipa Haule, kabla ya kumkuta Mayele aliyeukwamisha wavuni, akiiwezesha Yanga kuibuka na ushindi huo wa bao 1-0.

Goli hilo la jana la Mayele ni mwendelezo wa kuifungia timu yake mabao muhimu ambapo wiki iliyopita nyota huyo alikuwa na mchango mkubwa kwenye ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Marumo Gallants ya Afrika Kusini kwenye nusu fainali ya kombe la Shirikisho Afrika na kuisaidia Yanga kutinga hatua ya fainali ya michuano hiyo.

Ushindi wa jana dhidi ya Singida Big Stars unaipa Yanga tiketi ya kutinga fainali na sasa watavaana na 'Wanarambaramba', Azam FC kwenye fainali itakayochezwa kwenye Uwanja wa Mkwakwani mkoani Tanga.

Hata hivyo, Yanga tayari ni mabingwa wa Tanzania Bara na wana tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa kwa msimu ujao wa ligi.

Pamoja na hayo, nia ya viongozi na benchi la ufundi na wachezaji wa Yanga msimu huu ni kutwaa makombe matatu na tayari wanalo la ubingwa wa Ligi Kuu, huku tayari wakiwa kwenye fainali mbili, ikiwamo ya Kombe la Shirikisho barani Afrika walioingia Jumatano iliyopita na hili la FA.

Ushindi huo umeweka rekodi ya kutinga fainali mbili za michuano tofauti ndani ya wiki moja tu.

Katika mchezo wa jana licha ya mechi kuanza taratibu ilikuwa ikichangamka kadri muda ulivyozidi kusonga mbele, kwani dakika ya tisa tu, Mbrazil Bruno Gomes alipenyezewa pasi ndefu kutoka kwa Paschal Wawa, akawazidi mbio mabeki wa Yanga na kupiga krosi ambayo hata hivyo iliishia kwenye mikono ya golikipa Metacha Mnata.

Dakika kumi baadaye, Bruno alikosa bao la wazi baada ya kuruka juu kuunganisha kwa kichwa mpira krosi iliyopigwa na Nickson Kibabage huku kipa Metacha akiwa ameshaenda maboya, mpira huo ulitoka nje kidogo ya lango.

Mbrazili huyo aliendelea kuwa mwiba kwa safu ya ulinzi ya Yanga ambapo dakika ya 27 aliwatoka mabeki wa Yanga, akawafungasha tena, kabla ya kuachia shuti kali lililodakwa na Metacha licha ya kumponyoka kabla ya kuuwahi tena na kuudaka.

Baada ya mashambulizi hayo makali ya Singida Big Stars ni kama Yanga waliamka wakiongozwa na

INAENDELEA UKURASA 23



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, akinyanyua mikono juu kushangilia bao pekee aliloifungia timu yake jana dhidi ya Singida Big Stars kwenye nusu fainali ya kombe la FA, Uwanja wa Liti mkoani Singida. **PICHA: BINZUBERY**

## Viongozi Simba waingia 'msituni'

**Na Saada Akida**

WAKATI kukiwa na majina ya wachezaji wanaohusishwa kusajiliwa na Simba, uongozi wa klabu ya Simba umesema kwa sasa upo 'msituni' wakijipanga kwa ajili ya usajili wa nguvu.

Hivi karibuni Simba imeanza kuhusishwa na majina ya nyota wazawa, Edmund John wa Geita Gold FC, Yahya Mbegu wa Ihefu pamoja na nyota wa kimataifa, mshambuliaji wa Vipers ya Uganda, Milton Karisa huku pia uongozi wa Simba ukidaiwa kutenga kiasi cha dola150,000 kwa ajili ya kumsajili kiungo mkabaji kutoka nchini Ethiopia akitumikia klabu ya St George, Yiech Gatoch Panom.

Simba imetenga kiasi hicho ili kufanikisha mpango wa kufanya maboresho katika kikosi chake, huku baadhi ya wachezaji wakitajwa kujiunga na timu hiyo kwa ajili ya msimu ujao wa 2023/24 ambao umepangwa kuanza baadaye mwezi Agosti.

Katika nafasi ambazo Simba wamepanga kuziboresha kwa kusajili wachezaji ni safu ya kiungo mkabaji inayochezwa na Sadio Kanoute, Mzamiru Yassin, Jonas Mkude na Ismael Sawadogo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema bado suala la usajili linabaki kuwa siri ya uongozi na benchi la ufundi kwa kuwa ligi bado haijamalizika na kwa sasa viongozi wanaendelea kupitia ripoti ya benchi la ufundi waliokabidhiwa kwa ajili ya kufanya maboresho ya kikosi chao.

Alisema yapo baadhi ya majina ya wachezaji wapo nao katika mazun-

INAENDELEA UKURASA. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >